KUCHUNGUZA UKAHABA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MIFANO KATIKA VUTA N'KUVUTE NA TATA ZA ASUMINI

SAUMU JUMA KHAMIS

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUKIDHI MASHARTI YA KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo **Uchunguzi wa Ukahaba katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano katika *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini.*** Na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dkt. Hadija Jilala

(Msimamizi)

Tarehe: ----------

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yeyote ile, iwe kazi nzima au sehemu ya kazi hii bila kibari cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma ya Uzamili na Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba ya mwandishi, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeleo ya kitaaluma.

TAMKO

Mimi, **Saumu Juma Khamis,** nathibitisha kwamba Tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya masharti ya kupata yoyote.

Saini

Tarehe

IKIRARI

Tasnifu hii ni nakala halisi ambayo imehifadhiwa na hairuhusiwi kwa mtu yeyote kunakili au kuiga kazi hii, isipokuwa wale wanaofanya utafiti, kujisomea au kufanya mapitio ya maandishi, bila idhini ya mwandishi wa Tasnifu hii, au na Mkurugenzi wa masomo ya Uzamili na Uzamivu, kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wazazi wangu; baba yangu Bw. **Juma Khamis Issa** na mama yangu Bi. **Siti Khamis Bakar** kwa malezi bora waliyonipa mtoto wao na kunipa elimu. Namuomba Mwenyezi Mungu awape uzima na afya njema ili wafaidi matunda ya kazi yao kwangu.

SHUKURANI

Awali kabisa, nianze kwa kumshukuru **Allah Subhanahu Wataa'la** kwa kunijaalia afya njema, uzima na uvumilivu wakati wote wa masomo yangu na utafiti huu. Bila shaka huu ulikuwa wakati mzito ambao michango na misaada ya hali na mali ya watu mbalimbali ilihitajika. Nitakuwa si binadamu ninayejali utu, iwapo sitawashukuru watu mbalimbali ambao kwa namna moja ama nyingine walichangia masomo yangu na ukamilishaji wa utafiti huu. Ingawa si rahisi kubainisha wote kwa majina kwani ni wengi, lakini nitawataja wachache miongoni mwao ili wawe ni wawakilishi wa wengine.

Kwanza, napenda kushukuru kwa dhati msimamizi wangu Dkt. Hadija Jilala kwa msaada wake mkubwa wakati wa usimamizi wa utafiti na uandishi wa tasnifu hii. Aliniongoza kuandaa pendekezo la utafiti na mchakato mzima wa utafiti na uandishi wa Tasnifu. Bila shaka, ni kwa usimamizi wake uliojaa busara na hekima ndio kazi hii ikaonekana katika sura ilivyo hii leo. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie uzima na afya njema na ampe wepesi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Aidha, shukurani za pekee kwa walimu na wanafunzi wenzangu wa Umahiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tawi la Zanzibar kwa ushirikiano walionipa kipindi chote cha masomo na utafiti huu. Bila kuwasahau watoa taarifa walionipatia data ya uwandani katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Ushirikiano walionipa umetoa mafanikio makubwa katika kukamilisha utafiti huu.

Vilevile, nitakuwa mwizi wa fadhila endapo nitasahau kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia; mume wangu Bwana Masoud Said Suleiman na watoto wetu Said, Munir, Aisha, Muhsin na Asma kwa upendo na uvumilivu mkubwa waliouonesha

wakati wote wa masomo na katika kipindi chote cha utafiti huu. Uvumilivu wao ulinipa matumaini na utulivu wa kuendelea na masomo yangu vizuri. Zaidi ya yote, namshukuru kwa dhati mume wangu kwa kuniruhusu kuendelea na masomo yangu. Nasema shukurani jaziila, Mwenyezi Mungu akuzidishie taufiki hapa na pengine. Mwisho, itakuwa ni muhali kwangu kusahau kutoa shukurani kwa jamaa zangu dada na kaka zangu wote. Kwa hakika wao walinipa moyo pale nilipokata tamaa na kunipa matumaini na kunielekeza njia za mafanikio.

IKISIRI

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza suala la Ukahaba katika riwaya ya Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini*. Pia, malengo mahususi ya Tasnifu hii ni matatu; ambayo ni kubainisha usawiri wa Ukahaba na wahusika makahaba katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini,* kulinganisha sababu za Ukahaba zinazojitokeza katika riwaya hizo na uhalisia wake katika jamii na kuonyesha athari za Ukahaba kwa wahusika na jamii kwa ujumla.

Data za utafiti huu zimekusanywa kutoka maktabani na uwandani ambapo data za maktabani zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji maandiko na data za uwandani zimekusanywa kwa kutumia mbinu tatu za ukusanyaji data. Mbinu hizo ni majadiliano ya vikundi, usaili na hojaji. Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Saikochanganuzi zimetumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu.

Utafiti huu umebaini kuwa riwaya za Kiswahili zinatumia baadhi ya wahusika kusawiri suala la Ukahaba. Usawiri huu unadhihirisha uhalisia uliomo katika jamii na jinsi riwaya za Kiswahili zinavyowasilisha suala la Ukahaba na mtazamo wa jamii kuhusu Ukahaba. Aidha, utafiti umebaini sababu kadhaa za Ukahaba zilizojibainisha kutoka kwenye riwaya teule na zilizowasilishwa na wanajamii. Sababu hizo ni pamoja na umasikini, starehe, mazoea, kwenda na wakati, na ukosefu wa malezi. Pia, utafiti umegundua kwamba Ukahaba una athari kwa wahusika na jamii kwa ujumla. Zaidi ya hayo, utafiti huu umebaini kuwa waandishi kwa kiasi kikubwa wanawatumia wahusika wa kike tu kuwasawiri kama makahaba japokuwa kwa kiasi fulani wasanii hao wameshindwa kuwahusisha wahusika wa kiume moja kwa moja kama makahaba.

YALIYOMO

Ukurasa

ITHIBATI i

HAKIMILIKI ii

TAMKO iii

TABARUKU v

SHUKURANI vi

IKISIRI viii

YALIYOMO ix

SURA YA KWANZA 1

UTANGULIZI WA JUMLA 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Utafiti 1

1.3 Tatizo la Utafiti 3

1.4 Malengo ya Utafiti 4

1.4.1 Lengo Kuu 4

1.4.2 Malengo Mahsusi 4

1.5 Maswali ya Utafiti 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti 5

1.7 Upeo wa Mada ya Utafiti 5

1.8 Uzingatifu wa Maadili ya Utafiti 6

1.9 Muundo wa Tasnifu 9

1.10 Hitimisho 10

SURA YA PILI 11

KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA 11

2.1 Utangulizi 11

2.2 Fasili ya Dhana 11

2.3 Historia Fupi ya Riwaya ya Kiswahili Tanzania 12

2.3 Ukahaba katika Riwaya za Kiswahili 15

2.4 Tafiti kuhusu Ukahaba 18

2.5 Kiunzi cha Nadharia 22

2.6 Pengo la Utafiti 25

2.7 Muhtasari wa Sura 26

SURA YA TATU 27

MBINU ZA UTAFITI 27

3.1 Utangulizi 27

3.2 Eneo la Utafiti 27

3.3 Mbinu za Ukusanyaji wa Data 27

3.3.1 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi 28

3.3.2 Mbinu ya Usaili 28

3.3.3 Mbinu ya Hojaji 29

3.4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli 29

3.4.1 Walengwa wa Utafiti 29

3.4.2 Sampuli 30

3.4.3 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli 30

3.4.3.1 Usampulishaji Lengwa 30

3.4.3.2 Usampulishaji Nasibu 31

3.5 Vifaa vya Ukusanyaji wa Data 31
3.5.1 Daftari na Kalamu 32
3.5.2 Karatasi za Hojaji 32
3.5.3 Mwongozo wa Maswali 32
3.5.4 Kinasa Sauti 32
3.5.5 Kompyuta Pakatwa 33
3.5.6 Kamera 33
3.6 Uchambuzi wa Data 33
3.7 Muhtasari wa Sura 34
SURA YA NNE 35
UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA 35
4.1 Utangulizi 35
4.2 Muktasari wa Riwaya Teule 35
4.2.1 Vuta N'kuvute 35
4.2.2 Tata za Asumini 36
4.3 Usawiri wa Ukahaba katika Riwaya Teule 36
4.4 Uchambuzi wa Riwaya ya Vuta N'kuvute 37
4.4.1 Usawiri wa Ukahaba katika Vuta N'kuvute 38
4.4.2 Wahusika Wanaojihusisha na Ukahaba 41
4.4.2.1 Yasmin 41
4.4.2.2 Denge 43
4.4.2.3 Mwajuma 44
4.4.2.4 Mambo 45
4.4.3 Mtazamo wa Mwandishi kuhusu Ukahaba 45

4.5 Uchambuzi wa Riwaya ya Tata za Asumini 47
4.5.1 Usawiri wa Ukahaba katika Tata za Asumini 48
4.5.2 Wahusika Wanaojishughulisha na Ukahaba 50
4.5.2.1 Miriam 51
4.5.2.2 Zaina 52
4.5.2.3 Daddy 52
4.5.2.5 Sewa 53
4.5.3 Mtazamo wa Mwandishi kuhusu Ukahaba 54
4.6 Sababu za Ukahaba katika Riwaya na Jamii 56
4.7.2 Athari kwa Jamii 64
4.8 Mtazamo wa Jamii kuhusu Ukahaba 66
4.9 Hitimisho 68
SURA YA TANO 69
MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 69
5.1 Utangulizi 69
5.2 Muhtasari wa Mjadala wa Utafiti 69
5.2.1 Kujibu Maswali ya Utafiti 70
5.2.2 Mchango wa Utafiti 73
5.3 Hitimisho 74
5.4 Mapendekezo 75
MAREJELEO 77

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii inahusu utangulizi wa jumla ambapo inabainisha vipengele vya awali vya utafiti. Vipengele hivyo ni usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, fasili na ufafanuzi wa dhana mbalimbali, muundo wa tasnifu, uzingativu wa maadili ya utafiti na muhtasari wa sura.

1.2 Usuli wa Utafiti

Ukahaba ni mwenendo wa mwanaume au mwanamke kushiriki uasharati kama biashara yake, umalaya, utaleleshi, uzinifu na uzinzi (TUKI, 2004). Ukiachia mbali riwaya pendwa ambazo mara nyingi huakisi mapenzi, starehe na matukio mengine ya kusisimua, riwaya nyingi za Kiswahili zilizoandikwa baada ya uhuru na kuendelea hadi hii leo zinalenga kujenga jamii mpya kwa kuikosoa, kuionya na kwa kiasi fulani kuiburudisha jamii hiyo (Nguma, 2001).

Tunapozungumzia kuhusu mapenzi mara nyingi tunamaanisha mahaba aliyonayo mtu juu ya mtu mwingine au kitu. Kama tutakavyoona hapo baadaye kwamba mapenzi yamegawanyika katika pande mbili; ambazo ni mapenzi ya dhati na mapenzi yasiyo dhati. Mapenzi ya dhati siku zote hujenga amani na utulivu wa nyoyo za wapendanao ambapo mapenzi yasiyo ya dhati huzaa chuki na uhasama miongoni mwa wanajamii (Nguma, 2001). Kwa muktadha huo mapenzi ya dhati huleta athari chanya katika jamii na kinyume chake mapenzi yasiyo ya dhati huleta athari hasi katika jamii hiyo.

Kwa upande wa watunzi wa riwaya, nao huwasilisha masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii zao ambayo yanahusu nyanja tofauti za maisha ya wanajamii kama vile uwanja wa kisiasa, kiuchumi, kielimu, kijamii na kiutamaduni. Pia, dhamira ya mapenzi imekuwa ikijitokeza katika riwaya mbalimbali kwa watunzi kuwasawiri wahusika ambao hujishughulisha na mapenzi katika jamii. Mapenzi hayo hujadiliwa katika pande mbili, ambazo ni mapenzi ya dhati na mapenzi yasiyo dhati. Suala la Ukahaba huibuliwa kwenye mapenzi yasiyo ya dhati. Mara nyingi, wahusika makahaba huchukuliwa kuwa hawana mapenzi ya dhati kwa wale wanaoshirikiana nao kufanya ngono. Kupitia katika kazi za fasihi, mara nyingi wahusika wa kike huchorwa wakijishirikisha kufanya ngono kwa ajili ya kipato, kupanda cheo au kupata hadhi fulani ambapo wahusika wa kiume huonyeshwa wakifanya ngono kuridhisha miili yao. (Mhilu na wenzake, 2013). Kwa upande wa jamii, mara nyingi inapozungumziwa dhamira ya mapenzi kwa wahusika moja kwa moja, hadhara hurejelea kwenye mahusiano yanayofungamana na ngono miongoni mwao. Japokuwa wenye mahusiano hayo tunaweza kuwaita wapenzi, lakini si kila wapendanao huwa wana mahusiano ya kingono. Kwa hiyo, dhamira ya mapenzi ni pana ikilinganishwa na inavyochukuliwa na watu wengine (Senkoro, 1982).

Kwa kuwa, Ukahaba ni suala ambalo huhusishwa na mapenzi ambayo hujitokeza kwa namna tofauti katika jamii, waandishi wa riwaya nao huisawiri dhamira hii katika kazi zao. Hata hivyo, matarajio yetu ni kwamba waandishi hao wangeusimulia Ukahaba kulingana na uhalisia wake katika jamii, bila kuongeza au kupunguza chochote. Hivyo basi, utafiti huu ulichunguza dhamira ya Ukahaba katika riwaya zilizoteuliwa ili kubaini iwapo dhamira hii inawasilishwa kulingana na uhalisia uliopo ndani ya jamii au kuna ukengeushi wa kiasi fulani unaofanywa na watunzi wa

riwaya. Pia, utafiti huu ulikusudia kubaina kufanana na kutofautiana kwa mitazamo ya watunzi wa riwaya wanaposawiri dhamira inayofanana katika kazi zao. Riwaya hizo zimechaguliwa kwa sababu ndani yake suala la Ukahaba linajitokeza katika vitabu hivyo na wahusika wamechorwa wakijishughulisha na Ukahaba kama sehemu ya maisha yao. Mtafiti alisoma vitabu hivyo na kubaini usuli wa awali. Hivyo vitabu hivyo viliteuliwa ili kufanya utafiti wa kina zaidi.

1.3 Tatizo la Utafiti

Ukahaba katika kazi za fasihi ya Kiswahili ni dhamira ambayo haijafanyiwa tafiti za kutosha. Baadhi ya tafiti ambazo zimefanyika kuhusu riwaya ni Senkoro (1982) ambaye alitafiti suala la Ukahaba katika fasihi ya Kiafrika; Hata hivyo utafiti wa Senkoro katika makala hiyo ni wa jumla na si mahsusi. Mlacha, (1984) aliyehakiki dhamira ya ujenzi wa jamii mpya katika riwaya za Visiwani; na Onwukwe (1988) aliyechunguza dhamira za malezi katika riwaya za Kezilahabi. Hawa ni baadhi tu ya watafiti walioshughulikia dhamira katika riwaya ya kiswahili. Pamoja na kuwa hakuna tafiti za kutosha kuhusu Ukahaba katika fasihi. Suala hili limeandikwa na Senkoro (1982) ambaye katika makala yake amechunguza Ukahaba katika fasihi ya kiafrika. Ilionekana kuwa kuna haja ya kufanya utafiti wa kina katika fasihi ya kiswahili hususani utanzu wa riwaya kuhusu Ukahaba. Kwa hiyo tatizo la utafiti huu ni kuchunguza Ukahaba unavyojitokeza katika riwaya ya kiswahili kwa kutumia Riwaya ya *Vuta N' kuvute* na *Tata za Asumini* ili kubaini uhalisia wa Ukahaba katika fasihi ya kiswahili. Kwa kadri ya uelewa wa mtafiti, licha ya jitihada za watafiti hao na wengine, suala la Ukahaba katika riwaya za Kiswahili za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* halijatafitiwa kabisa.

Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza suala la Ukahaba katika riwaya za Kiswahili kwa kulinganisha hali inayosimuliwa katika riwaya hizo na uhalisia wake katika jamii. Riwaya za *Vuta N'kuvute* (Shafi, 1999) na *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990) ni kazi teule ambazo zilichaguliwa kutumika katika utafiti huu. Riwaya hizo zimechaguliwa kwa sababu ndani yake suala hilo la Ukahaba linajitokeza kwa watunzi kuwaonesha baadhi ya wahusika wakijihusisha na Ukahaba kama sehemu ya maisha yao.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo ya aina mbili; ambayo ni lengo kuu na malengo mahususi. Malengo hayo yalikuwa kama ifuatavyo hapa chini:-

1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza suala la Ukahaba katika riwaya ya Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* kwa kulinganisha na uhalisi wake katika jamii.

1.4.2 Malengo Mahsusi

Ili kufikia lengo kuu utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi yafuatayo:

(1) Kubainisha usawiri wa Ukahaba na wahusika makahaba katika Riwaya za *Vuta N'Kuvute* na *Tata za Asumini.*

(2) Kulinganisha sababu za Ukahaba katika Riwaya za *Vuta N'Kuvute* na *Tata za Asumini* na uhalisia katika jamii.

(3) Kuonyesha athari za Ukahaba kwa wahusika na jamii.

1.5 Maswali ya Utafiti

Katika kuhakikisha kwamba malengo hayo yafikiwa kwa ufanisi, utafiti huu ulijielekeza kujibu maswali yafuatayo:-

(1) Kuna usawiri gani wa Ukahaba na wahusika makahaba katika Riwaya za *Vuta N'Kuvute* na *Tata za Asumini?*

(2) Sababu za Ukahaba katika Riwaya za *Vuta N'Kuvute* na *Tata za Asumini* zinafanana na kutofautianaje na mtazamo wa jamii?

(3) Kuna athari gani za Ukahaba zinazowapata wahusika na jamii?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkubwa kijamii na kifasihi. Hii ni kwa sababu utakuwa ni wa kwanza kuchunguza kwa kina Ukahaba katika riwaya za Kiswahili za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* ambazo zilichaguliwa. Pia, utafiti huu umelinganisha na dhamira ya Ukahaba inayowasilishwa katika riwaya hizo na uhalisia wake katika jamii. Zaidi ya hayo, utafiti huu utakuwa dira na mwongozo kwa watafiti wengine watakaochunguza zaidi kuhusu dhamira hii. Pia utatoa mchango wa kitaaluma wa kuielimisha jamii kuhusu athari za Ukahaba sambamba na kutoa mapendekezo ya namna ya kupunguza athari hizo. Kwa ujumla, utafiti huu una umuhimu mkubwa katika uwanja wa fasihi na uwanja wa jamii.

1.7 Upeo wa Mada ya Utafiti

Kimsingi utafiti huu ulikusudia kuchunguza usawiri wa Ukahaba katika riwaya za Kiswahili. Lakini kulingana na uchache wa muda uliopangwa kwa ajili ya utafiti na uhaba wa fedha za kufanyia utafiti,ijapokuwa suala la Ukahaba limezungumziwa

katika tanzu mbalimbali za fasihi, utafiti huu ulijikita kuchunguza suala la Ukahaba katika riwaya mbili zifuatazo:

i) Riwaya ya *Vuta N'kuvute* (Shafi, 1999) na
ii) Riwaya ya *Tata za Asumini* (Mohamed, 1990)

Uteuzi wa riwaya hizi ulifanywa kwa sababu wakati mtafiti alipokuwa anasoma riwaya mbalimbali za Kiswahili aliona kuwa katika riwaya hizi, suala la Ukahaba limejitokeza kwa uwazi na kwa kubaini wahusika mbalimbali wanaojihusisha na Ukahaba. Hivyo, kupitia utafiti huu tukachunguza usawiri wa Ukahaba na kulinganisha yaliyoandikwa katika kazi hizo na uhalisia wake katika jamii ya Waswahili.

1.8 Uzingatifu wa Maadili ya Utafiti

Padgett (2002), anaeleza masuala ya kimaadili ambayo yanaweza kujitokeza na ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika aina zote za utafiti. Masuala hayo ni pamoja na kuomba idhini na ruhusa ya kufanya utafiti katika eneo la utafiti, usiri, uwazi, ushiriki wa hiari kwa wahojiwa, utiifu na uvumilivu.

Katika sehemu hii tumeeleza masuala ya kimaadili ambayo mtafiti anatakiwa kuyazingatia katika utafiti wake kabla ya utafiti kuanza, wakati wa utafiti na baada ya kukusanya data. Kwa kuwa utafiti huu ulihusisha watu kutoka maeneo mbalimbali na mtafiti kutembelea taasisi mbalimbali za kiserikali na kibinafsi, na kila sehemu ina taratibu zake hivyo mtafiti alipaswa kuzingatia maadili ya utafiti.

Hivyo basi, mtafiti kabla ya kuanza kufanya utafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kibali ambacho kilimwezesha kupewa kibali kutoka mamlaka inayohusika na utoaji wa vibali vya utafiti kwa upande wa Zanzibar.

Kibali hicho kilimsaidia mtafiti kuingia katika maeneo yote ya utafiti wake na kumlinda kisheria. Wakati akiwa maeneo husika mtafiti kabla ya kuwaona watafitiwa aliwaona viongozi wenye mamlaka katika maeneo hayo. Kwa hiyo, mtafiti alifika kwa masheha wa shehiya ili kujitambulisha kwa kuonesha kibali cha utafiti na kuwatoa wasiwasi juu ya uwepo wake na shughuli iliyomsukuma kuwepo hapo.

Baada ya kupata ridhaa ya kuanza kazi ya utafiti mtafiti aliomba ridhaa kwa washiriki wake bila ya kuwalazimisha na wale waliokataa kushiriki aliwaachia. Pia, watu hao aliwaridhia kwa upole bila ya kuwalazimisha, kwani Kombo na Tromph (2006), wanaeleza kuwa ni muhimu sana washiriki wa utafiti wakashiriki kwa kujitolea bila kulazimishwa. Hivyo washiriki wote waliotoa data walitoa kwa hiari yao. Mtafiti aliwaeleza watafitiwa lengo la utafiti wake, kuanzia lengo kuu na kwa nini anahitaji data hizo mpaka matarajio yake, ili kupata maoni ya watafitiwa. Baada ya kutoa lengo la utafiti wahojiwa waliuliza maswali ya kutaka ufafanuzi juu ya suala la Ukahaba. Hivyo, mtafiti alitoa maalezo ya kina na watafitiwa wakaridhika juu ya hilo, hii ilisaidia kurahisisha zoezi zima la utafiti ambapo wahojiwa walioshiriki katika kutoa data za utafiti huu, walitoa data hizo kwa hiari na kwa uamuzi wao bila kutenzwa nguvu na mtafiti. Wakati wa kukusanya taarifa mtafiti aliuliza maswali yake kwa usahihi na kwa sauti ili kufahamika kwa urahisi na kuweka kumbukumbu za taarifa zote katika sehemu husika.

Kwa vile utafiti huu ulitumia kinasa sauti ambacho kilitumika kurekodi mahojiano kati ya mtafiti na wahojiwa. Kabla ya kutumia zana hii, mtafiti aliomba ridhaa ya washiriki. Mtafiti aliwaeleza wahojiwa sababu na umuhimu wa kutumia zana hizi na kuwaomba ridhaa ya kuitumia. Wahojiwa walikubali na kuwa tayari kurekodiwa

katika kinasa sauti hicho. Kutokana na uwazi huu alioufanya mtafiti kwa watoa taarifa ulimsaidia katika kukusanya data na kufanya zoezi hilo kuwa rahisi. Data za zilizo kusanywa kwa njia ya mahojiano na usaili zilihifadhiwa katika kinasa sauti ili kuweza kurejelewa pale mtafiti alipohitaji.

Mtafiti pia, alizingatia suala la usiri kwa kuwaahidi na kuwahakikishia washiriki waliotoa taarifa za utafiti huu kuwa data walizozitoa zitakuwa ni siri ya mtafiti na mhojiwa na kutumika kwa ajili ya malengo ya utafiti huu tu na si vinginevyo. Kwa kufanya hivyo, wahojiwa hawakutakiwa kutaja majina yao wakati wa kutoa taarifa ili kulinda siri ya mtoa data. Kwa kulinda ahadi hii ya usiri mtafiti aliyoitoa kwa wahojiwa wake, matokeo yote ya utafiti huu hakuna urejelezi wa jina la mtoa taarifa lilitoandikwa katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Kama wanavyoeleza Kombo na Tromph (2006) kwamba, washiriki hawanabudi kuhakikishiwa na watafiti kuwa usiri wa data wanazozitoa utazingatiwa. Hii ni pamoja na kuwahakikishia kuwa, data hizo hazitatumika vinginevyo zaidi ya kutimiza malengo ya utafiti huu na bila kubainisha chanzo cha data hizo.

Sambamba na hayo, suala la faragha lilizingatiwa wakati wa ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa. Kwa sababu mtafiti alitambua kuwa kila mshiriki ana haki ya kupata faragha. Watafitiwa wengine walitaka usaili ufanyike majumbani kwao hasa wazee, mtafiti aliamua kuwafuata huko majumbani kwao kwa ajili ya kupata ufaragha na kupata data za uhakika kwani mtafiti alipofuata matakwa ya mtafitiwa aliweza kujiskia kuwa yuko huru na kutoa data za uhakika.

Vilevile, sayansi ya utafiti umezingatiwa na kufuatwa kuanzia kabla ya kukusanya data, wakati wa ukusanyaji wa data, baada ya ukusanyaji wa data na katika

uchambuzi wa data. Mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu zimezingatia misingi ya kufanya uchunguzi wa sayansi jamii.

1.9 Muundo wa Tasnifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza inabainisha utangulizi wa jumla unaohusu mada ya utafiti ambapo mambo yanayojadiliwa katika sura ya kwanza ni pamoja na usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, na mawanda ya utafiti fasili na ufafanuzi wa dhana mbalimbali. Pia sura hii inaeleza juu ya muundo mzima wa tasnifu hii na uzingatifu wa maadili wakati wa kufanya utafiti.

Pia, sura ya pili inaeleza juu ya mapitio ya maandiko na machapisho mbalimbali kuhusu mada ya utafiti tunayoichunguza. Katika sura hii, dhana muhimu zinazotumika katika utafiti huu zimefafanuliwa kwa ufupi na kwa umakini mkubwa. Dhana hizo ni pamoja na; Ukahaba, umalaya, uzinifu na mapenzi. Pia, katika sura ya pili tumeeleza juu ya nadharia iliyotuongoza katika kukusanya na kuchambua data zetu za utafiti.

Aidha, sura ya tatu inahusu mbinu mbalimbali na njia tulizozitumia katika mchakato mzima wa ukusanyaji data na uchambuzi wa data hadi kufikia matokeo ya utafiti wetu. Vilevile tumeeleza eneo la utafiti ambako data zilizotumika katika utafiti huu zilipatikana na kufanyiwa kazi.

Sura ya nne ni ya uchambuzi. Ni sura ambayo inaonesha uwasilishaji wa data za utafiti, uchambuzi wa data hizo na mijadala mbalimbali ya taarifa kuhusiana na suala

la Ukahaba katika riwaya ya Kiswahili nchini Tanzania. Pia, katika sura hii matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa upana wake.

Sura ya tano ndio ya mwisho katika tasnifu hii ambapo inahusu muhutasari wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo ya mtafiti kwa ajili ya kuboresha fasihi ya Tanzania hususani katika uandishi wa riwaya. Pia sura hii ina mapendekezo kwa ajili ya tafiti zitakazoendelea katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili Tanzania.

1.10 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza utangulizi wa jumla kuhusu mada ya utafiti, usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti ambayo ndiyo yaliyosimama kama mwongozo wa utafiti huu. Zaidi ya hayo katika sura ya kwanza tumejadili umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na mpangilio wa Tasnifu nzima na maadili ya utafiti. Sura itakayofuata itaelezea mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia.

SURA YA PILI

KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunajadili kazi tangulizi mbalinbali kuhusu tafiti za riwaya ambazo zinaelezea dhamira ya Ukahaba. Sura hii ina utangulizi, fasili ya dhana na historia fupi ya riwaya ya Kiswahili. Pia sura hii inaelezea dhamira ya tahakiki za riwaya za Kiswahili, tafiti kuhusu Ukahaba, kiunzi cha nadharia, pengo la utafiti na muhtasari wa sura.

2.2 Fasili ya Dhana

Katika sehemu hii tumefasili na kufafanua baadhi ya dhana au maneno muhimu ambayo yametumika katika utafiti huu. Miongoni mwa maneno ambayo yamefasiliwa ni pamoja na Ukahaba, uasherati, umalaya, na uzinifu.

Kwa mujibu wa TUKI (2004) *Ukahaba* ni mwenendo wa mwanaume au mwanamke kushiriki tendo la uasharati kama biashara yake, umalaya, uzinifu au uzinzi. Kupitia kamusi hiyo maneno hayo manne; yaani *Ukahaba*, *umalaya*, *uzinifu* na *uzinzi*, yametumika kama visawe kwa maana kwamba unapolitumia neno moja miongoni mwao unarejelea maneno hayo. Hivyo, fasili iliyotolewa na TUKI kuhusu Ukahaba inarejelea pia uasherati, uzinifu na uzinzi. Kwa kiasi fulani tunakubaliana na fasili hiyo ya TUKI isipokuwa tunaweza kuongeza kwa kusema kuwa Ukahaba ni tendo la kufanya ngono nje ya ndoa yaani uhusiano unaokubalika katika jamii, tena na watu mbalimbali na kwa malipo. Mtendaji anayepokea malipo ya Ukahaba huitwa kahaba au malaya ambapo mshiriki anayetoa malipo huitwa mteja. Aidha, mshiriki wa ngono huitwa mzinzi au mzinifu.

Kimsingi kuna aina mbili kuu za Ukahaba kutegemea na mhusika anavyojishirikisha katika tendo la Ukahaba (Senkoro, 1982). Kwanza, mshiriki anaamua kujifanyia kazi mwenyewe na namna kujipatia wateja. Huyu mara nyingi anapatikana akitembea barabarani, kusubiri kwenye mabaa au kwa kutangaza namba ya simu katika mitandao ya kijamii na kadhalika. Anaweza pia kujitangaza kwa kurusha picha kupitia wavuti za intaneti na kukutana na wateja mahali mbalimbali. Pili, mshiriki anafanya kazi chini ya usimamizi wa mtu mwingine au watu wengine. Hali yake inaweza kufanana na aina fulani ya ajira ya kulipwa ambapo mhusika hulipwa na msimamizi anayepokea fedha kwa kila tendo la ngono au mhusika anatakiwa kutoa malipo fulani kwa msimamizi kutokana na mapato yake. Kahaba wa aina hii mara nyingi hupatikana katika danguro lakini pia anaweza kupatikana barabarani katika maeneo maalumu. Katika kundi hili kuna aina ya utumwa wa kingono ambako mabinti na wanawake wanalazimishwa kujiuza kwa wateja ambapo msimamizi wa ngono au mtu ambaye huwaunganisha wanawake hao kwa wanaume huitwa *Kuwadi*.

Pamoja na fasili na ufafanuzi huo kuhusu dhana ya Ukahaba, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba wanajamii hawajifungi na dhana kwamba Ukahaba ni kufanya tendo la ngono kwa malipo tu. Kwa mujibu wa watoa taarifa wetu, vitendo vya uzinifu na uzinzi pia huchukuliwa kama Ukahaba.

2.3 Historia Fupi ya Riwaya ya Kiswahili Tanzania

Kuna wataalamu na waandishi mbalimbali wa fasihi ambao wametafiti kazi mbalimbali za riwaya za Kiswahili na hata riwaya za kigeni. Baadhi ya kazi tangulizi ambazo tumezipitia kuhusu tafiti za riwaya za Kiswahili ni kama zinavyoonekana hapa chini. Lakini kabla hatujazijadili kazi hizo ni vyema tuangalie kwa ufupi

historia ya riwaya za Kiswahili nchini Tanzania. Historia hiyo inaonekana kama ifuatavyo:

Mara nyingi fasihi hufungamana na maendeleo ya jamii tukimaanisha kwamba jamii ndiyo inayoibua na kuendeleza fasihi. Kadri jamii hiyo inavyoendelea katika nyanja mbalimbali za maisha ndivyo tanzu tofauti tofauti za fasihi zinavyojitokeza na kupewa nguvu. Mara nyingi tunaelezwa kuwa chimbuko la riwaya za Kiswahili ni ngano simulizi ambapo wakati wa jioni au usiku wa mapema mababu au mabibi na wajukuu wao walikaa pamoja kusimuliana ngano (Madumulla, 1988). Ikiwa huo ndio msingi riwaya andishi za Kiswahili, kama zinavyofahamika siku hizi, zimeingia baada ya ukoloni. Hata hivyo, zina asili katika fasihi simulizi ya jamii za Waswahili kifani na kimaudhui (Njogu & Chimerah, 2008).

Kwa hakika, riwaya za Kiswahili katika kipindi kifupi cha maisha yake zimeweza kupata maendeleo makubwa. Hata hivyo, historia yake ina utata kidogo kuhusu ipi ndiyo riwaya ya kwanza (Njogu & Chimerah, wameshatajwa). Ingawa watafiti wengi wanachukulia kuwa riwaya ya Kiswahili ilianza kipindi cha ukoloni wa Waingereza. Wachunguzi walio wengi wanachukulia kuwa riwaya ya kwanza kabisa ni *Uhuru wa Watumwa* iliyotungwa na James Mbotela mwaka 1934. Kuanzia miaka ya 1950 walijitokeza waandishi mahiri mbalimbali wa riwaya za Kiswahili. Miongoni mwa waandishi hao ni Shaaban Robert aliyeandika riwaya za *Kusadikika* (1951) na *Adili na Nduguze* (1952). Pia, katika miaka ya 1960, Shaaban Robert aliandika riwaya nyingine kama *Utu Bora Mkulima* (1966), *Maisha yangu na baada ya Miaka Hamsini* (1966) na *Siku ya Watenzi Wote* (1968). Maudhui makubwa ya riwaya za wakati huo yalihusu zaidi maadili na masuala ya kidini. Pia maudhui yenye kuonesha

mivutano iliyokuwepo baina ya watawala wa kikoloni na Waafrika ilibainishwa katika riwaya hizo za awali.

Aidha, kwa mujibu wa Madumulla (1988), riwaya zilizoandikwa kwenye miaka ya 1970 zilijihusisha na maudhui ya ujenzi wa jamii mpya kama vile uongozi na usaliti wa kisiasa; pia, katika kipindi hiki ndicho ambacho inasemekana kuwa riwaya za kisasa ziliibuka. Waandishi wengi chipukizi walijitokeza kuandika riwaya. Miongoni mwao ni Kezilahabi aliyeandika *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), Mohamed Suleiman aliandika *Kiu* (1972), *Nyota ya Rehema* (1978) na *Kivumbi Uwanjani* (1978) na Senkoro aliandika *Mzalendo* (1977).

Madumulla (ameshatajwa) anaendelea kueleza kuwa katika kipindi cha miaka ya 1980 riwaya za Kiswahili zilianza kuukaribia uhalisia wa kisanaa. Taratibu za maisha kama vile siasa na dini zilianza kutazamwa kwa jicho kali na udhaifu wake ulifichuliwa.

Pia, dhamira kama hizi zilizidi kushamiri katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa kwenye miaka ya 1990 hadi 2000. Katika vipindi hivyo, waandishi mbalimbali wa riwaya wamekuwa wakisawiri dhamira mbalimbali zenye kufichua maovu yaliyomo katika jamii (Mabala, 1993). Riwaya nyingi zilizoandikwa zilijielekeza kwenye dhamira kuu ya ujenzi wa jamii mpya. Kwa sababu baada ya uhuru jamii zetu zimekabiliwa na changamoto mbalimbali katika nyanja zote za maisha kama vile kisiasa, kijamii, kiuchumi, kielimu na kiutamaduni. Katika uwanja wa kisiasa, kwa mfano, waandishi wamekuwa wakifichua uovu unaofanywa na viongozi wa jamii zetu baada ya kupata uhuru. Baadhi ya riwaya ambazo ziliandikwa miaka ya 1990 ni

Tata za Asumini (1990) iliyoandikwa na Said A. Mohamed na *Vuta N'kute* (1999) iliyoandikwa na Shafi Adam.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), riwaya za Kiswahili zilizoandikwa katika vipindi mbalimbali zinajibainisha kifani na kimaudhui kiasi kwamba zimeufanya utanzu huu wa fasihi uwe na wapenzi wengi zaidi ukilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi andishi ya Kiswahili. Kwa mfano, katika riwaya hizi miongoni mwao kuna kazi zenye maudhui mazuri ambayo yanajenga jamii kwa kusawiri maisha halisi ya jamii zinazohusika. Wanajamii wanapaswa kuzitumia kazi za fasihi kama kioo cha kujitazamia na kujisahihisha kila ambapo panaonekana kuwa na kasoro. Licha ya hayo, kuna baadhi ya riwaya hususani riwaya pendwa ambazo hujikita moja kwa moja kusawiri dhamira za mapenzi, upelelezi na ujambazi,; dhamira ambazo badala ya kujenga jamii kimaadili, maudhui yake yanaipotosha jamii hiyo. Kupitia riwaya pendwa vijana hupata hamasa ya kujishirikisha na masuala ya ngono, wizi na vitendo vingine ambavyo ni kinyume na maadili ya jamii zetu.

2.3 Ukahaba katika Riwaya za Kiswahili

Kuanzia miaka ya 1980 walijitokeza watafiti, wahakiki na wataalamu mbalimbali wa fasihi ambao wametafiti, kuhakiki na kujadili riwaya mbalimbali za Kiswahili na zisizo za Kiswahili. Katika sehemu hii tumeangalia baadhi ya wataalamu na watafiti wa fasihi ya Kiswahili ambao wametafiti kuhusu riwaya za Kiswahili, baadhi ya watafiti hao ni kama wafuatavyo hapa chini:

Senkoro (1982) alitafiti suala la Ukahaba katika fasihi ya Kiafrika. Katika kazi hiyo, Senkoro anabainisha jinsi ambavyo waandishi wa kazi za fasihi katika bara la Afrika wanavyosawiri wahusika wakijishughulisha na suala la Ukahaba katika kazi zao.

Senkoro anaendelea kueleza kuwa bali ya suala hili kusawiriwa katika kazi za fasihi pia Ukahaba umeshamiri katika jamii nyingi za Kiafrika. Kwa mfano, katika baadhi ya jamii za Kiafrika, wanawake wanajihusisha na Ukahaba kwa kuuza miili yao ili waweze kukidhi mahitaji yao ya maisha. Licha ya kujadili dhamira hiyo ya Ukahaba, kazi ya Senkoro haikujikita katika riwaya za Kiswahili pekee badala yake alitumia kazi mbalimbali za fasihi zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili, Kifaransa na Kiingereza. Kwa hiyo, kazi hiyo inaweka pengo kwa upande wa dhamira ya Ukahaba katika riwaya za Kiswahili. Hivyo, utafiti huu umechunguza suala la Ukahaba mahususi katika riwaya za Kiswahili kwa kulinganisha yanayoelezwa katika vitabu na uhalisia wake katika jamii.

Naye, Mlacha, (1984) alitafiti dhamira ya ujenzi wa jamii mpya katika riwaya za visiwani. Hizi ni riwaya ambazo zimeandikwa na waandishi kutoka visiwa vya Zanzibar ambazo pia usawiri wa wahusika na mandhari katika kazi hizo zinahusu visiwa vya Zanzibar. Katika kazi hiyo, Mlacha anajadili dhamira za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya katika visiwa vya Zanzibar. Anabainisha kuwa licha ya kuwa katika miaka ya 1950 na 1960 jamii za Wazanzibari na Watanzania kwa jumla zilikuwa katika haraka za kupigania uhuru kwa ajili ya kuzikomboa jamii hizo kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, pamoja na kupatikana kwa uhuru huo lakini uhuru wa kweli haujafikiwa. Mpaka hivi sasa jamii ya visiwani imo katika uozo kwenye nyanja mbalimbali za maisha kiasi kwamba uhuru wa kweli haujafikiwa. Licha ya kuchunguza dhamira ya ujenzi wa jamii mpya, kazi yake haijashughulikia dhamira ya Ukahaba katika jamii hiyo. Kazi hiyo inatupa ombwe la kitaaluma kuhusu dhamira ya Ukahaba. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza suala la

Ukahaba katika riwaya za Kiswahili zilizoteuliwa kwa kulinganisha yanayoelezwa katika vitabu na uhalisia wake katika jamii.

Pia, Onwukwe (1988) alitafiti suala la malezi katika riwaya za Euphrase Kezilahabi. Katika utafiti wake, Onwukwe alibaini kwamba katika riwaya za Kezilahabi malezi yanaweza kugawanywa katika sehemu kuu mbili. Kwanza, kuna malezi bora yanayoendana na mila, utamaduni na desturi za Mtanzania. Pili ni malezi yasiyo bora ambayo yanavunja maadili na utamaduni wa Watanzania. Kwa mfano katika jamii aliyoichunguza alibaini kuwa watoto wengi katika jamii hizo hawana maadili mazuri badala yake wanajihusisha na vikundi viovu vya ulevi, Ukahaba na wizi. Ingawa imejadili kwa kina dhamira ya malezi, kazi ya Onwukwe haijajadili kabisa suala la Ukahaba katika riwaya za Kiswahili wala jamii inayohusika. Kutolichunguza suala hili panajitokeza pengo la maarifa ambalo linahitaji kufanyiwa kazi. Hivyo basi, utafiti huu umechunguza suala la Ukahaba katika riwaya za Kiswahili kwa kulinganisha yanayoelezwa katika vitabu na uhalisia wake katika jamii.

Aidha, Nguma (2001) alichunguza taswira ya mwanamke namna inavyochorwa katika riwaya mbalimbali za Kezilahabi. Katika utafiti wake, Nguma alibaini kuwa mwanamke katika riwaya amechorwa kwa taswira za tofauti tofauti. Mathalani, mwanamke amechorwa kwa taswira chanya na hasi. Kwa upande wa taswira chanya, mwanamke ameonyeshwa kama mshauri wa mwanaume katika masuala ya kijamii na kifamilia na mwanamke kama mchapakazi katika jamii. Kwa upande wa dhamira hasi mwanamke amechorwa kama chombo cha starehe na mwanamke kama mtu duni katika jamii za Afrika. Kwa ujumla, Nguma anafafanua kwamba Kezilahabi humchora mwanamke katika taswira za namna mbili kuu ambazo ni taswira yenye mtazamo chanya na taswira yenye mtazamo hasi. Pamoja na kumuonyesha

mwanamke katika dhamira mbalimbali, Onwukwe hakuligusia hata kidogo suala la Ukahaba katika kazi yake. Hali hiyo inaweka pengo kuhusu dhamira hii; pengo ambalo linahitaji kuzibwa. Hivyo basi, utafiti huu umechunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya za Kiswahili kwa kulinganisha yanayoelezwa katika vitabu na uhalisia wake katika jamii.

Mhilu, Nyangwine na Kanyuma (2013) walihakiki fani na maudhui katika riwaya ya *Takidini.* Katika uhakiki wao wanajadili dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika riwaya hiyo. Wanaeleza kuwa dhamira kuu ya riwaya hii ni ukombozi wa kiutamaduni katika jamii ya Watanzania. Pamoja na dhamira hiyo wanaelezea dhamira nyingine ndogo ndogo zinazojitokeza katika riwaya hizo kama vile mapenzi, ndoa, nafasi ya mwanamke katika jamii, umuhimu wa mshikamano, malezi ya watoto na kadhalika. Pamoja na kubainisha dhamira ya mapenzi katika kazi hiyo suala la Ukahaba hawajalijadili kabisa. Kutokulijadili suala hili wameweka pengo la kitaalamu ambalo linalohitaji kuzibwa. Hivyo basi, utafiti huu umechunguza dhamira ya mapenzi katika riwaya za Kiswahili kwa kulinganisha yanayoelezwa katika vitabu na uhalisia wake katika jamii.

2.4 Tafiti kuhusu Ukahaba

Katika sehemu hii tumejadili tafiti mbalimbali zilizochunguza suala la Ukahaba katika riwaya zisizo za Kiswahili. Miongoni mwa kazi ambazo zimeandikwa kuhusu suala la Ukahaba ni ya Smart (1976) ambaye alifanya utafiti kuhusu mwanamke na uhuni. Smart katika utafiti wake ameueleza Ukahaba kwa msisitizo mkubwa ambapo ameanza kwa kuelezea mitazamo mbalimbali kuhusu Ukahaba. Pia, amegusia nadharia za kisaikolojia na mitazamo ya kijamii kuhusu Ukahaba. Halikadhalika, amefafanua namna Ukahaba unavyoonekana kama suala la wanawake tu na sio la

wanaume. Katika utafiti wake anamtazama mwanamke kama kahaba peke yake na kutomzingatia mwanaume. Pia, mtazamo wa Smart kuhusu Ukahaba ni kwamba hiki ni kitendo cha kuvunja sheria, kanuni na kaida za jamii. Kwa mujibu wa utafiti wa Smart (1976), kahaba anastahili kupewa adhabu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufungwa jela.

Naye, Senkoro (1982). Senkoro amechunguza kuhusu Ukahaba katika fasihi ya Kiafrika kwa kuhusisha jamii mbalimbali za Waafrika. Katika kazi hiyo, Senkoro ametumia riwaya za fasihi ya Afrika zilizoandikwa kwa lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Kifaransa. Tukichunguza kwa makini tunabaini kuwa mtazamo wa Senkoro umejikita zaidi upande wa waandishi ambao wameshughulikia suala hili katika bara la Afrika. Anaendelea kufafanua kuwa kuna waandishi ambao wanamsawiri kahaba kama kiumbe potovu ambaye hana matumaini ya kuendelea katika maisha. Amewabainisha baadhi ya waandishi kama vile Mohamed (1972), Sadji (1958). Hata hivyo, Senkoro anawaeleza kuwa waandishi hawa wanaligusia kijuujuu mno suala la Ukahaba katika kazi zao. Wengi wao hawaliongelei kwa undani na kuechambua sababu zinazowaingiza wasichana na wanawake wengi katika Ukahaba.

Hata hivyo, utafiti wa Senkoro umetofautiana na utafiti huu kwa sababu utafiti wetu umeangalizia Ukahaba katika fasihi ya Kiswahili pekee badala ya fasihi ya Afrika. Pia, utafiti huu malengo yake ni tofauti na ule wa Senkoro, hivyo utafiti wetu umebaini baadhi ya mambo ambayo ni tofauti na yale yaliyobainishwa na utafiti wa Senkoro. Mathalani, katika kazi hiyo Senkoro ameonyesha namna Ukahaba unavyojitokeza katika kazi ya fasihi na kulaumu tabaka la chini ambapo anamtazama kahaba kama mwakilishi wa tabaka la chini. Kuhusu hili utafiti wetu umebaini

kwamba si makahaba wote ambao ni wa tabaka la chini ambao ni duni kiuchumi. Kwa hiyo, kuna makahaba wengine ambao wanajiweza kiuchumi na wanafanya Ukahaba kwa kujiridhisha nafsi zao tu. Jambo jingine ambalo Senkoro hakuligusia kwa undani ni sababu zinazowavutia wasichana na wavulana wengi katika Ukahaba ambapo amebainisha sababu za kiuchumi tu bila kugusia sababu za kisaikolojia na kijamii ambazo tumezigundua katika utafiti wetu. Pia, katika kazi hiyo, Senkoro haoneshi nafasi ya wanaume katika kuendeleza Ukahaba katika jamii ambapo kwa kiasi kikubwa amejikita kwa wanawake.

Pia, Muga (1980) alifanya utafiti kuhusu Ukahaba katika nchi za Afrika Mashariki, Magharibi, Kusini, Zaire na Nevada. Katika utafiti wake ameanza kwa kujadili maana ya kahaba na Ukahaba. Kwa kina zaidi utafiti huo unajikita katika kuchambua masuala fulani yanayohusiana na Ukahaba kwa mfano kabila, umri, elimu, dini na uozo katika jamii. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa hatukujishughulisha na masuala ya umri, kabila, dini na kadhalika katika kuchambua suala la Ukahaba katika riwaya. Ingawa kwa kiasi fulani kazi ya Muga (1980) inabainisha suala la Ukahaba lakini kazi hiyo haionyeshi sababu zinazowafanya wasichana na wavulana kujiingiza katika Ukahaba; jambo ambalo limeonyeshwa katika utafiti huu.

Halikadhalika, Kishtainy (1982) amefanya utafiti kuhusu suala la Ukahaba na asili ya Ukahaba katika kazi za fasihi. Pia, anabainisha jinsi makahaba wa1ivyotumiwa katika mahekalu matakatifu huko Ugiriki. Kishtainy anaujadili Ukahaba katika jamii ambazo suala hilo limehalalishwa na linaonekana kama kazi ya kujipatia mapato ya juu kuliko kazi nyingine za ofisini. Katika kazi yake Kishtainy (1982:42) anafafanua kwa kueleza kuwa wanawake wengi hujiingiza katika kazi ya Ukahaba maana mapato yake ni mengi ku1iko kazi ya ofisini. Hali hii ambayo Kishtainy anausawiri

Ukahaba ni tofauti sana na ha1i tuliyoibaini katika kazi za Shafi Adam na Said A. Mohamed. Kwa sababu makahaba wengi wasichana katika riwaya za Shafi Adam Shafi na Said A. Mohamed ni watu duni na wanafanya kazi ya kujipatia angalau mahitaji yao ya siku tu wala hakuoneshwa kahaba aliyepatia mapato makubwa kwa shughuli hiyo.

Utafiti mwingine ulifanywa na Strobel (1975) ambao ulihusu mwanamke wa Kiislamu nchini Kenya. Anaeleza kwamba Ukahaba katika mji wa Mombasa ulianza mara tu baada ya utumwa kupigwa marufuku. Katika kipindi hicho wanawake wengi ambao walikuwa wamewekwa majumbani kama masuria na vimada iliwabidi wajiingize katika Ukahaba. Pia, anaendelea kufafanua kuwa wasichana wengi waliingizwa katika maisha ya Ukahaba na watalii pamoja na mabaharia waliofika katika mji wa Mombasa. Hata hivyo, kazi ya Strobel haiwezi kuitwa ya kifasihi, kwa sababu hakuna vitabu vya kifasihi ambavyo alivitumia kama marejeo. Kwa kiasi kikubwa utafiti wake ulijiegemeza katika imani ya kidini.

Vilevile, Little (1980) alichunguza kuhusu taswira ya mwanamke wa mjini katika fasihi ya Kiafrika. Katika kazi yake anajaribu kuonyesha jinsi waandishi wanavyowasawiri wanawake katika maisha ya mjini. Anabainisha namna ambavyo wasichana wengi ·wanavyopambana na maisha ya mji na hatimaye kujiingiza katika Ukahaba, uasherati na ulevi. Licha ya hayo, hajaeleza kwa nini maisha ya mjini yanawaathiri zaidi wanamke kuliko maisha ya vijijini na suluhisho la tatizo hili.

Zaidi ya watafiti hao, Bakwesegha (1982) amefanya utafiti kuhusu suala la Ukahaba nchini Uganda. Bakwesegha anajadili namna Ukahaba unavyoendeshwa katika mji wa Kampala. Katika kazi yake, Bakwesegha amejishughulisha na kubainisha aina

mbalmbali za makahaba wanaopatikana mjini Kampala. Pia, amebainisha mahali ambapo Ukahaba hufanyika. Ametaja baadhi ya mahali humo kuwa ni katika kilabu za usiku, mabaa na vyuo vya elimu ya juu. Aidha, anaelezea suala la ushoga kwa wanaume na wanawake katika kuendeleza Ukahaba miongoni mwa wanafunzi. Mwisho amebainisha wanaume mbalimbali ambao ni washiriki wa Ukahaba kama vile waliotengana na wake zao, wanaoishi mbali na familia zao na vijana wasijaooa.

Katika tafiti hizo ambazo zimepitia kuhusu suala la Ukahaba katika jamii mbalimbali zimeweza kubaini suala la Ukahaba limeenea katika jamii mbalimbali hapa ulimwengu. Aidha, kazi hizo zimetoa mwanga juu ya dhana, sababu na mitazamo ya wanajamii kuhusu Ukahaba. Kazi hizo kwa kiasi kikubwa zimemsaidia mtafiti na kumpatia mwamko kuhusu kujenga mjadala unohusu Ukahaba katika jamii.

2.5 Kiunzi cha Nadharia

TUKI (2004) wanafasili nadharia kuwa ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Nao, Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Wanaendelea kufafanua kwamba nadharia ni maelezo ya jambo kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo hilo. Pia, Mdee na wenzake (2011) wanaeleza kuwa nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Aidha, Jilala (2016) anaifasili nadharia kuwa ni wazo ambalo huibuliwa kama mwongozo kwa msomaji ama mchambuzi na hata mwanafasihi linganishi katika kutoa majumuisho ya kazi za fasihi na zisizo za fasihi. Kutokana na fasili hizo

tunaweza kusema kwamba nadharia ni kigezo kinachotumika kumuongoza mtu katika kuchunguza au kutathmini jambo.

Kwa kuwa Ukahaba ni suala lenye mawanda rnapana sana kiasi kwamba ha1iwezi kutathminiwa kikami1ifu kwa kutumia nadharia moja, hivyo tumetumia nadharia zaidi ya moja. Hii ni kwa sababu Ukahaba husababishwa na hali mbalimbali za kisaiko1ojia, kijamii, kiuchumi na hata kibayolojia. Kwa hiyo, utafiti huu umetumia nadharia mbili ambazo ni *Nadharia ya uhalisia* na *saikochanganuzi.* Nadharia hizi tumezifafanua kwa marefu na mapana hapa chini.

Nadharia ya Uhalisia.

Kwa mujibu wa Wellek (1961) dhana ya uhalisia inajihusisha na ukweli dhahania wa hali ya vitu ilivyobadilika na kuwa falsafa iliyoongelea vitu thabiti vinavyohusika na mishipa ya fahamu ya binadamu. Kwa mujibu wa historia, nadharia ya uhalisia wa kifasihi inaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha (Wafula na Njogu, 2007).

Katika nadharia hii, kazi ya fasihi inatakiwa ioneshe maisha ya binadamu jinsi yalivyo. Naye, Hegel, (1971) anaeleza kuwa uhalisia unahusu uigaji wa mazingira ambamo binadamu anaishi. Kwa mujibu wa Hegel, nadharia ya uhalisia inahusishwa na dhima, jukumu na wajibu wa mtunzi katika kubainisha ukweli jinsi ulivyo. Pia, uhalisia ni kama mbinu ya kisanii ambayo hujaribia ukweli. Mbinu hii ina mashiko katika kueleza na kujadili hali halisi ya maisha ya watu. Mbinu hii pia huonesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao katika kazi ya fasihi.

Nadharia hii imemsaidia mtafiti kutathimini namna waandishi wa kazi alizoziteua, walivyojibidiisha kuonesha ukweli kuhusu Ukahaba katika kazi zao ili kutoa picha

halisi ya mazingira ya jamii. Kwani wakati mwingine mwandishi anatakiwa kutoa picha halisi ya jamii bila kuikuza wala kuipunguza. Pamoja na hayo ni vyema tuelewe kwamba baadhi ya wakati si lazima mwandishi kuchora picha halisi ya jamii bali anaweza kujibidiisha kulingana na nadharia na mtindo alioutumia (Wafula na Njogu, 2007). Hivyo basi, nadharia hii imemuongoza mtafiti kulinganisha kilichoelezwa katika kazi za fasihi na uhalisi au ukweli wake katika jamii. Hali ambayo imemuwezesha mtafiti kuonyesha mtazamo wa waandishi na wanajamii kuhusu Ukahaba.

Kulingana na upana huu, nadharia yetu ya utekelezi ambayo tunaitumia kama mizani yetu haitoshelezi bila kuazima kutoka katika nadharia nyingine ambapo nadharia ya saikochanganuzi ya Freud (1974) imetumika.

Nadharia ya Saikochanganuzi

Nadharia hii inafanya uchanganuzi wa masuala ya kisaikolojia juu ya mambo mbalimbali yanayomkumba binadamu katika maisha yake. Kwa hiyo, nadharia hii imefaa kuelezea hali mbalimbali za kisaikolojia zinazochangia kuwaingiza wahusika wakike na wakiume katika Ukahaba. Kwa mfano, Freud (1974) anaeleza kwamba wanawake au wanaume wengi wanaojishirikisha katika Ukahaba ni wale ambao wana uchu zaidi wa mapenzi. Jambo ambalo huanzia utotoni wakati mtu anapoanza kumtamani mzazi wake. Kutokana na hali ya kukusanyika kwa uchu pamoja na kuendelea kupevuka kwa mwili wa binadamu huwafanya baadhi ya watu kuwa makahaba. Watu wenye udhaifu huu katika hutumia vitendo vya ngono kulipiza kisasi. Aidha, nadharia hii ya kisaikolojia inabainisha kwamba makahaba wengi hutokana katika familia ambazo haziko imara. Hivyo basi, makahaba wengi ni wale

watoto waliofiwa na wazazi, waliokosa malezi bora kutoka katika familia zao na jamii kwa ujumla. Kwa hakika nadharia ya kisaikolojia imetoa mchango mkubwa katika kubaini wahusika makahaba kwa sababu kuna makahaba katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* wanaonyesha udhaifu wa nafsi zao kisaikolojia kuliko udhaifu wa kiuchumi.

Kutokana na malengo ya utafiti huu, mtafiti ilimbidi kutumia nadharia zaidi ya moja kwa sababu aliiona kwamba nadharia ya Uhalisia pekee haiwezi kutosheleza mahitaji ya uchunguzi wa utafiti huu. Kwa hiyo, mtafiti aliongeza nadharia nyingine ambayo ilisaidia malengo ya utafiti huu. Nadharia ya saikolojia imesaidia kuchambua sababu zinazofanya baadhi ya wahusika kujishughulisha na Ukahaba ndani ya jamii. Kwa ujumla, nadharia hizi zimetusaidia katika mchakato mzima wa utafiti huu kuanzia, ukusanyaji wa data na uchambuzi wake.

2.6 Pengo la Utafiti

Licha ya kuwa kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu Ukahaba katika jamii, hadi hivi sasa kazi hizo hazijaziangazia suala la Ukahaba katika riwaya za Kiswahili na uhalisia wake katika jamii. Kazi nyingi zimechunguza Ukahaba katika riwaya zisizo za Kiswahili kwenye jamii nyingine za Kiafrika. Aidha, pamoja na waandishi kuingiza dhamira ya Ukahaba katika kazi zao hakuna utafiti uliofanywa kulinganisha yanayozungumzwa katika riwaya na uhalisi uliopo katika jamii. Jambo ambalo linatufanya tujiulize hivi waandishi wanachokiandika kwenye kazi zao kina uhalisia na hali ilivyo katika jamii au wanakengeuka uhalisia huo? Kutokana na hali hiyo, ni wazi kwamba utafiti unahitajika ili linganishi kati ya kinachozungumzwa kwenye riwaya na uhalisia wake kwenye jamii inayohusika. Hili ndilo pengo la kitaaluma

ambalo mtafiti alikusudia kuliziba. Hivyo basi, katika kujaribu kuliziba pengo hilo, utafiti huu umechunguza dhamira ya Ukahaba katika riwaya ya Kiswahili.

2.7 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii tumejadili kazi tangulizi mbalinbali kuhusu tafiti na riwaya ambazo zinaelezea dhamira ya Ukahaba ambapo tumeanza kwa utangulizi wa sura, dhana ya Ukahaba na historia fupi ya riwaya ya Kiswahili. Pia, sura hii imeelezea dhamira ya tahakiki za riwaya za Kiswahili, tafiti kuhusu Ukahaba, kiunzi cha nadharia, pengo la utafiti na muhtasari wa sura. Sura itakayofuata itahusu mbinu mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu za utafiti ambapo inabainisha na kueleza mbinu mbalimbali zilizotumika katika mchakato wa utafiti huu. Tumeanza kwa kubainisha eneo la utafiti, njia za ukusanyaji wa data, sampuli na mbinu za uteuzi wa sampuli, vifaa vya kukusanyia data, uchambuzi wa data na Muhtasari wa Sura.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu kwa kiasi kikubwa ni wa maktabani, ingawa kwa upande mwingine ulihusisha mbinu za uwandani. Maktaba zilizotumika ni maktaba za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Makavazi ya TATAKI, Maktabani Kuu ya Zanzibar na Maktaba ya Chuo Kikuu Huria. Katika mkatiba hizo mtafiti ilipata fursa ya kupitia machapisho mbalimbali kama vile; makala, majarida, vitabu, tasnifu na maandiko mengineyo yanayohusiana na mada ya utafiti huu. Maandiko hayo kwa namna moja ama nyingine yamesaidia kuichambua zaidi mada ya utafiti huu kiasi cha mtafiti kupata mwelekeo kuhusu usawiri wa Ukahaba katika riwaya ya Kiswahili. Mbali na eneo la maktabani, utafiti huu pia umetumia data za uwandani. Kuhusu uwandani, mtafiti alikusanya data katika shehiya za Bububu mashariki. Bububu magharibi na Kihinani katika wilaya ya Magharibi, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar. Maeneo hayo ndipo walipotoka watoa taarifa ambao walifanya majadiliano na mtafiti na wengine kujaza hojaji.

3.3 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kothari (2004) anaeleza kuwa mbinu za ukusanyaji wa data ni mbinu ambazo hutumiwa kukusanya taarifa za kiutafiti ambazo hutumiwa katika kutolea matokeo

ya jumla ya utafiti. Nao, Cohen na wenzake (2000) wanaeleza kuwa katika kukusanya data, hakuna mbinu moja peke yake ambayo inaweza kujitosheleza. Hivyo, wataalamu hawa wanapendekeza matumizi ya mbinu zaidi ya moja ili kufikia mahitimisho yanayofaa kwa sababu hakuna mbinu iliyotoshelevu. Kwa hiyo, matumizi ya mbinu zaidi ya moja husaidia kupunguza upungufu utakaojitokeza katika mbinu moja kwa kufidiwa na mbinu nyingine. Hivyo basi, katika utafiti huu, mbinu mbalimbali zimetumika katika ukusanyaji wa data ambazo zilitumika kujibu maswali ya utafiti. Mbinu zilizotumika ni pamoja na mbinu za majadiliano ya vikundi, hojaji na usaili.

3.3.1 Mbinu ya Majadiliano ya Vikundi

Mligo (2012) anaeleza kuwa kikundi cha majadiliano kuwa ni kikundi ambacho hukusudia kujadili suala moja ambalo huwahusu washiriki wote wa kikundi. Kikundi cha mahojiano hutakiwa kuhusisha watu wenye sifa zinazofanana, hutoa habari za kitaaluma na huwa na mjadala wao hulenga jambo moja mahususi. Katika utafiti huu tulikuwa na kikundi kimoja ambacho kilijumuisha wazee na vijana, wakike na wakiume. Mtafiti akiwa na watoa taarifa wake kwa pamoja walijadili sababu za Ukahaba na athari zake katika jamii. Mtafiti alifanya majadiliano nao kwa kutumia maswali ambayo aliyaandaa kwenye karatasi, na maswali mengine yaliibuka wakati wa mjadala. Mbinu hii ilichaguliwa kwa sababu tulihitaji kupata mawazo ya jamii kuhusu suala la Ukahaba ndani ya jamii yao na mtazamo wa wanajamii kuhusu suala hili.

3.3.2 Mbinu ya Usaili

Kwa mujibu wa Kothari (2004) usaili ni mbinu ya ukusanyaji wa data kwa kutumia maswali simulizi. Katika kutumia mbinu hii, mtafiti huwa na orodha ya maswali

ambayo huyatumia katika kuwahoji watoa taarifa wake. Aidha, maswali mengine huibuliwa wakati wa mahojiano hayo ili kupata taarifa ambazo zitasaidia mtafiti kupata taarifa muhimu za utafiti. Katika utafiti huu, mbinu hii ilitumika kuwahoji wanajamii mbalimbali ambao mtafiti aliamini wanaweza kumpatia taarifa muhimu za kiutafiti. Mbinu hii ilichaguliwa ili kuweza kudadisi na kuona iwapo wanajamii mmoja mmoja huwa wanazingatia suala la Ukahaba ndani ya jamii.

3.3.3 Mbinu ya Hojaji

Kauti (2013) anaeleza kuwa hojaji ni orodha ya maswali ambayo mtafiti huyaandaa kwa ajili ya kukusanyia data au taarifa katika utafiti. Pia, mbinu hii ni mahususi kwa watu wanaojua kusoma na kuandika kwa sababu hutakiwa kuijaza hojaji kwa njia ya maandishi. Mtafiti aliitumia sampuli ya watoa taarifa ishirini ambao aliwapa hojaji zenye maswali. Watoa taarifa hawa walizijaza kulingana na uelewa wao juu suala la Ukahaba na namna linavyosawiriwa katika riwaya teule. Kwa kawaida mbinu hii ilimsaidia mtafiti kukusanya taarifa nyingi kwa muda mfupi kuhusu Ukahaba.

3.4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Sehemu hii inaelezea walengwa wa utafiti, sampuli, na mbinu zilizotumika katika uteuzi wa sampuli ambayo ilitumika kutoa taarifa ya utafiti.

3.4.1 Walengwa wa Utafiti

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), walengwa wa utafiti ni kikundi cha watu, vitu au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzitumia katika utafiti wake. Kwa kuwa utafiti huu ulihusu suala la Ukahaba katika riwaya na uhalisia wake katika jamii, walengwa ni wanajamii. Katika utafiti huu makundi matatu ya wanajamii kutoka eneo la utafiti yalihusishwa katika kupata data za utafiti. Kundi la kwanza

lilikuwa ni mchanganyiko wa wazee na vijana ambao walifanya mahojiano ya kikundi na mtafiti, kundi la pili lilikuwa ni watu wazima mmoja mmoja ambao mtafiti alifika majumbani mwao kuwasaili na kundi la tatu lilikuwa la vijana pekee ambao walijaza hojaji.

Aidha, ijapokuwa utafiti umefanyika katika wilaya ya Magharibi, shehiya za Bububu Mashariki, Magharibi na Kihinani ni katika jamii hii ambamo mtafiti alifanya uteuzi wa sampuli. Hivyo basi walengwa hao wamewakilisha jamii ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

3.4.2 Sampuli

Kothari (2004) anaeleza kuwa sampuli ni kikundi fulani cha watu kilichomo ndani ya mkusanyiko wa watu ambacho mtafiti anaamini kwamba kikundi hicho kitampatia taarifa anazozihitaji kuhusu utafiti wake. Kwa sababu hiyo, mtafiti hulazimika kuteua sehemu ya wanajamii ambao huitwa kundi lengwa. Katika utafiti huu, mtafiti aliteua sampuli kutoka katika maeneo ya utafiti kwa kutumia mbinu za sampuli nasibu na sampuli lengwa. Katika utafiti huu, sampuli ya watu arobaini iliteuliwa.

3.4.3 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Kothari (2004) anafasili uteuzi wa sampuli kuwa ni kitendo cha kuteua washiriki au wawakilishi kutoka katika kundi kubwa la watu watakaosaidia kupata kwa data na taarifa nyingine za utafiti. Katika utafiti huu mtafiti ametumia usampulishaji lengwa na nasibu kama ifuatavyo hapa chini.

3.4.3.1 Usampulishaji Lengwa.

Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kuwa sampuli lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti ambayo hutoa uhuru wa kuteua mtoa taarifa ambaye hudhaniwa

kuwa ana taarifa muhimu zitakazosaidia kujibu maswali ya utafiti. Kwa vile si rahisi kuchunguza riwaya zote za Kiswahili, mtafiti ameteua riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini.* Pia, sampuli lengwa imetusaidia kuwapata wanajamii ambao wamesoma riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu ambapo watoa taarifa wanne wamehusishwa kutoa taarifa ya kila riwaya. Mbinu hii imemsaidia mtafiti kuteua sampuli ambayo imempatia data zinazofaa kufikia malengo ya utafiti.

3.4.3.2 Usampulishaji Nasibu

Kombo na Trump (2006) wanafasili sampuli nasibu kuwa ni sampuli ambayo kila mtu miongoni mwa kundi lengwa anayo nafasi sawa ya kuteuliwa katika sampuli itakayoshiriki kutoa taarifa za utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu hii kuteua kundi watu wazima ambao walimpatia data kuhusu mtazamo wa jamii kuhusu suala la Ukahaba. Kundi hili lilijumuisha wanawake na wanaume mbinu hii ilitumika kupata sampuli kwa rika zote yaani vijana na watu wazima. Uteuzi huu umefanyika kwa sababu sio rahisi kuwahoji wanajamii wote. Hata ile ya jamii ya wakazi wa Bububu na Kihinani pia ilihitaji sampuli ili kuwakilisha wanajamii wa eneo hilo.

3.5 Vifaa vya Ukusanyaji wa Data

TUKI (2004) wanafasili data kuwa ni taarifa au takwimu ambayo hutumiwa kuelezea au kuthibitisha hoja fulani. Vifaa vya kukusanyia data ni vifaa mbalimbali ambavyo hutumika katika kukusanya na kuhifadhi data za utafiti. Katika harakati za kukusanya data za utafiti huu tulitumia vifaa mbalimbali kama; kalamu na daftari, hojaji, kumpyuta pakatwa, kinasasauti na kadhalika.

3.5.1 Daftari na Kalamu

Kothari (2004) anaeleza kuwa kalamu na karatasi ni vifaa vya asili vya katika ukusanyaji wa data ya utafiti. Bila shaka vifaa hivi vitaendelea kutumika kwa miaka mingi ijayo. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia daftari na kalamu ambavyo vilimsaidia katika kuhifadhi kumbukumbu hasa wakati wa usaili na majadiliano ya vikundi. Pia, vifaa hivi vilitumika katika kuandika majina ya watoa taarifa na watu wengine walioshiriki katika majadiliano ya vikundi.

3.5.2 Karatasi za Hojaji

Hojaji ni karatasi za maswali ambazo zimeandaliwa na mtafiti kwa ajili ya kujazwa na watoa taarifa wake. Katika utafiti huu, karatasi za hojaji zilikusudiwa kujazwa na watoa taarifa ambao wana ujuzi wa kusoma na kuandika. Watoa taarifa hawa walijaza hojaji kutoa taarifa za utafiti kuhusu Ukahaba katika kipengele cha kulinganisha uhalisia wa kwenye riwaya na jamii.

3.5.3 Mwongozo wa Maswali

Mwongozo huu huwa na maswali ambayo huandaliwa na mtafiti kwa ajili ya kumuongoza wakati wa kukusanya data. Maswali haya humsaidia wakati wa kufanya majadiliano ya vikundi na watoa taarifa wake. Maswali ya mwongozo yamemsaidia mtafiti kufanya mahojiano baina yake na watoa taarifa za utafiti. Hata hivyo, maswali mengine yaliweza kuibuliwa kadri na mijadala ilivyoendelea.

3.5.4 Kinasa Sauti

Kwa mujibu wa TUKI (2004) kinasa sauti ni chombo kinachotumika kunasia sauti wakati wamaongezi. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia kinasa sauti kurekodi majadiliano ya vikundi na katika usaili na watoa taarifa. Aidha, kinasa sauti

kimemsaidia mtafiti kurekodi na kuhifadhi data hizo ambazo alizitumia katika mchakato wa uchambuzi wa data.

3.5.5 Kompyuta Pakatwa

TUKI (2004) wanafasili istilahi ya kompyuta kuwa ni mashine ya kielektroniki ya kuhifadhi na kuchanganua taarifa zilizoingizwa, kukokotolea na kuongoza mitambo. Pia, kwa upande wa kompyuta pakatwa, hii ni aina ya kompyuta inayoweza kubebeka kwa urahisi kutoka sehemu moja hadi nyingine ambayo huweza kupakatwa. Katika utafiti huu, kompyuta pakatwa ilimsaidia mtafiti wakati wa kuandaa pendekezo la utafiti, hojaji, maswali ya mwongozo kwa ajili ya usaili na majadiliano ya vikundi, kuhifadhi data zilizokusanywa, kuhifadhi data na kuandika ripoti ya utafiti.

3.5.6 Kamera

Kwa mujibu wa TUKI (2004) kamera ni kifaa kinachotumika kupiga picha na kurekodi picha tuli au za mjongeo ambazo huambatana na matendo. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia kamera dijitali ili kuwapiga picha watoa taarifa kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za utafiti huu.

3.6 Uchambuzi wa Data

Kothari (2004) anafasili uchambuzi wa data kuwa ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti unaohusika. Katika utafiti huu tulitumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ilitumika katika kuchambua data za utafiti.

Pia, mbinu ya uchambuzi wa kifasihi ilitumika katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Omari (2009) uchambuzi wa kifasihi ni mbinu inayomruhusu mtafiti kusikiliza au

kusoma kazi ya fasihi kwa lengo la kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo na kadhalika. Aidha, mbinu ya uchambuzi wa kifasihi ni mbinu ya uchambuzi wa data, ambayo humruhusu kutoa maelezo ya kina kuhusu data zilizokusanywa ili ziweze kujibu maswali ya utafiti na kufikia malengo ya utafiti unaohusika. Vilevile, kwa kuwa data za utafiti huu zimekusanywa kwa mkabala usio wa kiidadi, pia uchambuzi wa data za utafiti huu umefanywa kimaelezo. Kutokana na hali hiyo data zilizokusanywa, uwandani na maktabani, zimewekwa katika makundi na kisha kuwasilishwa ili kuweza kufikia malengo mahususi ya utafiti.

3.7 Muhtasari wa Sura

Sura hii imejadili mbinu za utafiti ambapo imebainisha na kueleza mbinu mbalimbali zilizotumika katika mchakato wa utafiti huu. Tumeanza kwa kubainisha eneo la utafiti, njia za ukusanyaji wa data, sampuli na mbinu za uteuzi wa sampuli, vifaa vya kukusanyia data, uchambuzi wa data na mwisho ni Muhtasari wa Sura. Sura itakayofuata inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data ambapo data zilikusanywa kutoka makitabani na uwandani. Pia, inabainisha suala la Ukahaba lilivyosawiriwa katika riwaya na uhalisia wake katika jamii, sababu za wahusika kujiingiza katika uhakaba na athari za Ukahaba kwa wahusika na jamii kwa jumla na mwisho ni muhtasari wa sura.

4.2 Muktasari wa Riwaya Teule

Katika utafiti huu vitabu teuli ni riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini*. Katika sehemu zinazofuata tumebainisha riwaya hizo kwa kutoa maelezo mafupi kuhusu riwaya hizo ili kuwatoa muhutasari wake kwa wasomaji ambao hawajawahi kuzisoma, kuzihakiki au kuzichambua.

4.2.1 *Vuta N'kuvute*

Riwaya ya *Vuta N'kuvute* iliandikwa na Shafi Adam Shafi, mwaka 1999. Riwaya hii imejikita katika mapenzi na mapinduzi katika hali ya Vuta N'kuvute ya mambo hayo. Riwaya hii imeakisi mandhari ya kisiwa cha Unguja huko Zanzibar. Ina sura kumi na nane zilizopangiliwa vizuri ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Dhamira kuu ya riwaya hii ni umuhimu wa mabadiliko na ukombozi wa jamii katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Riwaya hii pia inawasilisha vuta nikuvute za maisha zinazomkabili Yasmin, msichana wa Kihindi aliyeozeshwa mume asiyemtaka, kwa nguvu za wazazi wake. Yasmin anamkataa mume wake Bwana Raza, mzee wa umri sawa na baba yake.

Yasmin anatoroka kutoka Mombasa anakoishi na mume wake na kurudi kwao Zanzibar (Masebo na Nyangwine, 2003). Kwa kitendo hicho Yasmin anafukuzwa nyumbani na wazazi wake na anasitiriwa na shoga yake, Mwajuma na kumuingiza Uswahilini.

4.2.2 *Tata za Asumini*

Riwaya ya *Tata za Asumini* iliandikwa na Said A. Mohamed, mwaka 1990. Riwaya hii imejikita katika kuonyesha hali ya misukosuko ya hali ya maisha yanayomkabili mhusika mkuu wa riwaya hii aitwaye Asumini. Riwaya hii imeakisi mandhari ya Uswahilini ambapo ina sura kumi na tatu zilizopangiliwa vizuri ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Dhamira kuu ya riwaya hii ni umuhimu wa mabadiliko na ukombozi wa jamii katika nyanja za kijamii na kiutamaduni.

Riwaya hii pia inawasilisha matatizo yaliyopata Asumini alipoishi katika hosteli za Chuo Kikuu, yeye akiwa ni mwanagenzi wa dunia chafu na ngumu ambaye anaonekana kunaswa na tata tokea mwanzo hadi mwisho wa riwaya hii. Ndani ya nafsi ya Asumini kuna mchocheo unaomtaka aendelee kufuata malezi mema aliyoyapata kwao na asikubali kunajisiwa. Lakini nje ya nafsi ya Asumini kuna mchocheo unaomchochea Asumini awe mchafu kama wachafu wengine.

4.3 Usawiri wa Ukahaba katika Riwaya Teule

Sehemu hii inajadili lengo mahususi la kwanza ambalo ni kubainisha usawiri wa Ukahaba na wahusika makahaba katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* ambazo ni riwaya teule katika utafiti huu. Kabla hatujajadili lengo hilo ni vyema kuelewa kwamba uchambuzi wa maudhui wa riwaya hizi umezingatia dhamira mahususi inayohusiana na utafiti huu ambayo ni suala la Ukahaba katika riwaya za

Kiswahili na uhalisia wake kwenye jamii. Uchanganuzi wa dhamira hizi umefanywa kwa kutumia nadharia za *Uhalisia* na *Saikochanganuzi* ambazo zimetuongoza kujua ukweli kuhusu Ukahaba na athari zake kwa jamii.

Hata hivyo, dhamira nyingine sio kwamba hazikutajwa kabisa bali zimebainishwa kila ilipobidi kufanya hivyo. Data za sehemu hii zimekusanywa wakati mtafiti alipokuwa anahakiki kazi teule na maoni ya watoa taarifa wa uwandani. Ufuatao hapa chini ni uchambuzi wa vitabu teule vya riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* ambapo katika uchambuzi huo tunalenga kubainisha usawiri wa Ukahaba na wahusika makahaba katika riwaya hizo*:*

4.4 Uchambuzi wa Riwaya ya *Vuta N'kuvute*

Vuta N'kuvute ni riwaya iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi, ambayo ilichapishwa mnamo mwaka 1999. Kwa ujumla riwaya hii imebainisha masuala ya mapenzi na mapinduzi katika hali inayoonesha vuta ni kuvute ya mambo katika jamii hiyo. Riwaya hii ya *Vuta N'kuvute* kwa uwazi kabisa inabainisha mandhari ya kisiwa cha Unguja katika Zanzibar. Riwaya hii ina jumla ya sura kumi na nane zilizopangiliwa vyema na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa wasomaji wake na jamii kwa jumla. Dhamira kuu ya riwaya hii ni kubainisha umuhimu wa mabadiliko na ukombozi wa jamii katika nyanja mbalimbali za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Pia, riwaya hii inawasilisha mivutano ya maisha yanayoomkabili mhusika mkuu wa riwaya hii, Yasmin. Yasmin ni mwanamke wa Kihindi ambaye aliozeshwa mume asiyempenda, ambapo aliozeshwa mume huyo kwa nguvu za wazazi wake. Yasmin anamkataa mume wake Bwana Raza, mzee wa umri wa miaka sabini. Bwana Raza alikuwa na umri sawa na umri wa baba yake Yasmin. Kutokana na hali hiyo, Yasmin

anatoroka Mombasa alikokuwa anaishi na mume wake na kurudi kwao Zanzibar (Masebo na Nyangwine, 2003). Kwa sababu hiyo, Yasmin anafukuzwa nyumbani kwa wazazi wake na anasitiriwa na rafiki yake, Mwajuma ambaye anamuingiza Uswahilini.

Akiwa katika maisha ya Uswahilini, Yasmin anakutana na Denge ambaye anaamua kumpenda sana lakini Denge mwenyewe hapendeki kwani saa zote alionekana yumo katika mapambano na wakoloni na makachero wake ili kuleta mabadiliko ya kisiasa nchini. Hata hivyo, Yasmin anafanya Ukahaba na Denge hadi kufikia kupata mimba na hatimaye anazaa mtoto. Dhamira hii ya Yasmin kufanya Ukahaba ndiyo tuliyoishughulikia katika utafiti huu.

4.4.1 Usawiri wa Ukahaba katika *Vuta N'kuvute*

Suala la Ukahaba katika riwaya hii halikusawiriwa kwa mapana na marefu yake kama ulivyo katika jamii. Usawiri wa Ukahaba katika riwaya ya *Vuta N'Kuvute* unajitokeza pale mwandishi anapowaonesha wahusika wake; Yasmin na Denge wakifanya mapenzi kwenye nyumba anayoishi Denge (uk. 73). Kama naharia yetu ya Uhalisia ya Walleck ni kawaida kwa wapenzi wa nje ya ndoa na ni jambo rahisi kwa mtu kumwambia mpenzi wake kuwa anampenda sana na waendelee kufanya mapenzi. Hivyo dhamira hii inauhalisia katika jamii zetu.

Pia, tunaoneshwa jinsi wanaume wasivyowaamini wanawake wanaotembea nao kwa njia ya Ukahaba. Kwani mara nyingi wanaume huwachukulia wanawake makahaba kuwa ni rahisi kugawa ngono kwa mtu yeyote. Kwa mfano, tunamuona Denge ambavyo hakuamini moja kwa moja pale alipoambiwa kuwa Yasmin ana mimba na mimba ile ni yake. Suala hili halipingani na Uhalisia katika jamii, kama nadharia

yetu inavyoeleza kuwa, kazi za fasihi hueleza picha halisi ya yote yaliyo katika jamii bila kuficha.

Aidha, tumeona jinsi wanaume wanavyokwepa kuwasaidia wanawake wanaofanya nao Ukahaba hata pale wanapobeba mimba. Kwa mfano, siku chache baada ya kupewa taarifa ya mimba, Denge alisafiri kwenda ng'ambo katika shughuli zake za kisiasa. Akiwa safarini hakuwa na habari tena kuhusu mimba ya mpenzi wake. Yasmin aliendelea kulea mimba peke yake huku akimuwaza mpenzi wake Denge akiwa na matumaini kuwa atakuwa tayari kumuoa. Hayo yanabainishwa na mwandishi uk.170 pale Yasmin anapomueleza rafiki yake Mwajuma anaposema:

> *... tumuombe Mungu anijaalie nijifungue salama na hata wakati huo naamini Denge atakuwa amekwisharudi, popote alipokwenda, nitamshauri nimsikilize ataniambia nini (kuhusu ndoa).*

Dondoo hilo linatubainishia matarajio ya wanawake wengi ya kutaka kuolewa na wanaume wanaofanya nao Ukahaba na kuwapa mimba. Hata hivyo, wanaume wengi, kama anavyoonekana Denge, wanakuwa hawapo tayari kuwaoa wanawake hao. Wanapotakiwa watoe kauli ya kukubali kufunga ndoa hukwepa kusema ukweli. Mwandishi (uk.182) anafafanua:

> *Denge unanipenda? Yasmin aliuliza, ...*
>
> *Kwa nini unaniuliza hivyo?*
>
> *Kwani kukuuliza hivyo vibaya? Palikuwa na kimya cha muda kidogo halafu Yasmin akaendelea, Nilikuwa nikikusubiri kwa muda mrefu nikuulize kama kweli unanipenda, kama uko tayari kuishi na mimi, kama utanioa.*

Denge hakuwa na la kujibu alinyamaza kimya kwa muda halafu alisema, Hata nikitaka kukuoa Yasmin, uwezo wa kuishi na mke sina.

Dondoo hilo linatubainishia kuwa Denge aliporudi safarini Yasmin alikuwa tayari amekwishajifungua lakini alipoombwa na mpenzi wake wapange kufunga ndoa hakuwa tayari kwa madai kwamba hana uwezo.

Hali hiyo pia imo ndani ya jamii yetu wanaume hukwepa kufunga ndoa na wanawake wanaofanya nao mapenzi kwa njia ya Ukahaba. Aidha, baadhi ya wanaume wanapopewa taarifa kuwa wanawake zao wamepata waume wa kufunga nao ndoa basi hukubali kwa urahisi. Hayo yanadhihirishwa na mazungumzo baina ya Yasmin na Denge. Dondoo lifuatalo (uk.183). linadhihirisha:

...akitokea mtu kutaka kunioa utakuwa radhi nikikubali kuolewa?

... N'takutakia kila la heri na mafanikio katika ndoa yako, alijibu Denge bila kufikiri.

Kulingana na dondoo hilo tunaweza kuona kuwa mara nyingi wanaume wanaotembea na wanawake kwa njia ya Ukahaba, wanafanya hivyo kujiridhisha hisia za miili yao kwani hawako tayari kufunga ndoa na wanawake hao. Hali hii imo katika jamii yetu kwani baadhi ya wanaume huwakana na hata kuwatelekeza wanawake zao wanaofanya nao Ukahaba mara tu wanapogundua kwamba wanawake hao wamepata ujauzito au matatizo mengine. Freud (1974) anaeleza kwamba wanawake au wanaume wengi wanaojishirikisha katika Ukahaba ni wale ambao wana uchu zaidi wa mapenzi, hivyo hukana na kukwepa majukumu yao hasa malezi

na mahitaji mengine kwani lengo lao la kufanya ngono kisaikolojia lilikuwa ni kukidhi matamanio ya miili yao.

Hata hivyo, kuna wanaume wengine huzikubali mimba zilizobebwa kuwa ni za kwao lakini wanaume hao hawako tayari kufunga ndoa na wapenzi wao kwa madai kwamba hawana uwezo wa kuwahudumia wanawake hao (Muga, 1980). Kutokana na hali hiyo, uchunguzi wetu unaonesha kwamba wanaume wengi hawako tayari kufunga ndoa na wanawake waliofanya nao Ukahaba kwa sababu kuu mbili. *Kwanza*, wanaume wengi wanaotembea nje ya ndoa hufanya hivyo ili kutekeleza matakwa ya hisia za miili yao tu. Hivyo wanaume kama hao kwao kuoa si jambo muhimu na wanaona kuwa watapata mzigo wa kuhudumia familia. *Pili*, baadhi ya wanaume hukataa kufunga ndoa na makahaba kwa sababu kuoa kahaba anayejulikana ni kitendo cha aibu au fedheha katika jamii. Kwa hiyo wanakataa kufunga ndoa ili kukimbia aibu kwa kuonekana wameoa wanawake wasio waaminifu.

4.4.2 Wahusika Wanaojihusisha na Ukahaba

Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute,* mwandishi amewachora baadhi ya wahusika wake wakijihusisha na suala la Ukahaba kwa namna tofauti. Katika riwaya hii tumeangalia wahusika wanne ambao ni Yasmin, Denge, Mwajuma na Mambo. Tuangalie wasifu wa wahusika hao katika sehemu zitakazofuata.

4.4.2.1 Yasmin

Yasmin ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Vuta N'kuvute.* Yasmin ni msichana wa Kihindi ambaye kwa wasifu wa nje, alikuwa na uso mdogo wa duwara na macho

makubwa na mwenye sura na umbile la kuvutia. Wasifu wa Yasmin unabainishwa na mwandishi uk.1 katika dondoo lifuatalo:

> *Yasmin alikuwa na kijiuso kidogo cha mdawari mfano wa tungule na macho makubwa ambayo kila wakati yalionekana kama yanayolengwa lengwa na machozi. Alikuwa na pua ndogo, nyembamba na chini ya pua hiyo ilipangana midomo miwili mizuri iliyokuwa haitulii kwa tabia yake ya kuchekacheka, huku akionesha safu mbili za meno yake mazuri. Alikuwa na kichaka cha nywele nyeusi zilizokoza ambazo zilianguka kwa utulivu juu ya mabega yake. Alikuwa si mrefu lakini hakuwa mfupi wa kuchusha, na matege aliyokuwa nayo yalizidi kuutia haiba mwendo wake wakati anapotembea.*

Kwa upande wa wasifu wa ndani, Yasmin amechorwa kama ni mwanamke aliyekutana na *vuta nikuvute* la kimaisha. Kwani akiwa ni kigoli wa miaka kumi na tano, mara tu baada ya kuvunja ungo, Yasmin aliozeshwa kwa mume asiyemtaka kwa nguvu za wazazi wake. Mume aliyemwoa Yasmin alikuwa wa umri karibu sawa na wa baba yake Yasmin. Hali hii ilimfanya Yasmin kumkataa mume wake, Bwana Raza, na kutoroka Mombasa walikokuwa wakiishi kurudi Unguja.

Kitabia, Yasmin ni mwanamke anayependa mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Kutokana na tabia hiyo ndio maana aliamua kumwacha mume wake wa kwanza; Raza, aliyelazimishwa na wazazi wake kuolewa naye. Aidha, Yasmin alikuwa anapenda kuwa na uhuru wa kuchagua mchumba wake mwenyewe na hakupenda wivu usio na maana. Kwa sababu hiyo ndipo akamkimbia Shihab kutokana na wivu wake.

Kwa ujumla, Yasmin ni mwanamke mvumilivu na jasiri sana. Alipingana na mila na desturi zilizopitwa na wakati katika jamii yake kama vile utabaka, ubaguzi wa rangi na ukandamizaji wa kijinsia. Kutokana na uvumilivu na ujasiri huo, aliweza kuyavumilia maisha magumu aliyoishi kwa Mwajuma licha ya vituko na shida mbalimbali alizopambana nazo. Kwa upande wa tabia nzuri tunaweza kusema kuwa Yasmin anafaa kuigwa na wanawake wengi katika jamii ya Watanzania.

4.4.2.2 Denge

Denge ni miongoni mwa wahusika wakuu katika riwaya ya *Vuta N'kuvute.* Yeye ni kijana wa Kiswahili ambaye kwa wasifu wa nje, alikuwa mwembamba, mrefu, rangi ya maji ya kunde, mwenye mwili mkakamavu. Wasifu kamili wa Denge tunauona pale aliposifiwa na mwandishi uk.47 katika dondoo lifuatalo hapa chini:

> *.. mrefu aliyezipata futi sita... wembamba uliojaa ukakamavu. Umbile ... na ile rangi yake ya maji ya kunde lilimfanya aonekane kama morani wa Kimasai. Macho yake madogo lakini makali... pua yake ilikuwa ya wastani na chini yake yalichipua masharubu machanga... na ndevu zilikuwa ndio Kwanza zinachipua... hayo yadhihirisha wazi umri wake mdogo, labda ndio Kwanza anapindukia miaka ishirini.*

Dondoo hilo linatubainishia wasifu wa nje wa Denge. Kwa upande wa wasifu wa ndani, Denge anaonekana shujaa, mzalendo na mwana mapinduzi. Siku zote yumo katika harakati ya kuleta mabadiliko ya kiutawala. Yuko mbioni kutaka kuiangusha serikali ya kikoloni ili kuondoa dhuluma, ubaguzi na ukandamizaji ulioendeshwa na

serikali hiyo. Matumaini ya Denge ni kuwa wazawa waweze kujitawala wenyewe kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Denge amechorwa kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Yasmin na anapendwa sana na Yasmin lakini hapendeki. Kwa Denge maisha ni mapambano na wakoloni tu na makachero wake. Kutokana na hali hiyo Denge hakuwa tayari kumsaidia mpenzi wake kwa lolote wakati wa ujauzito wala kulea mtoto akidai kwamba hana uwezo. Riwaya hii inamchora Denge kama kiwakilisho cha wanaume kama yeye ambao wapo katika jamii yetu (Masebo & Nyangwine, 2003). Wanaume hao wanawapenda wanawake kwa ajili ya kuwatekelezea matamanio yao ya kimwili tu, lakini hawako tayari kuwasaidia wapenzi wao wanapopatwa na matatizo.

4.4.2.3 Mwajuma

Mwajuma ni muhusika mmojawapo katika riwaya ya *Vuta N'Kuvute* ambaye amechorwa kama mwanamke mrembo anayeishi bila kufanya kazi badala yake anategemea Ukahaba kuendesha maisha yake. Mwajuma ameoneshwa kuwa na mahusiano ya kingono na Mambo ambapo Mambo huja nyumbani kwa Mwajuma kufanya mapenzi.

Kwa upande wa wasifu wa ndani, Mwajuma amechorwa kama ni mwanamke aliyekutana na maisha ya kawaida yasiyo rahisi wala magumu. Kwani akiwa ni kigoli wa miaka kumi na sita, baada ya kuvunja ungo, Mwajuma anahama kijijini kwao na kuhamia mjini ambako anaanza maisha kwa kufanya Ukahaba na wanaume tofauti tofauti ili aweze kuendesha maisha yake ya kila siku. Hali hii ilimfanya kuwa na mahusiano na wanaume kadhaa. Hata hivyo, Mwajuma anaonekana kuwa na roho

mzuri na moyo wa huruma. Alimpokea rafiki yake, Yasmin baada ya kufukuzwa na wazazi wake pale alipomkataa mumewe bwana Raza.

4.4.2.4 Mambo

Mambo ni muhusika katika riwaya hii ya *Vuta N'kuvute* ambaye hakujitokeza sana. Kwa upande wa wasifu wa ndani, Mambo anaonekana shujaa, mzalendo na mwana mapinduzi. Naye anashirikiana na rafiki yake Denge kutaka kuiangusha serikali ya kikoloni ili kuondoa dhuluma, ubaguzi na ukandamizaji ulioendeshwa na serikali hiyo. Matumaini ya Mambo ni kuwa wazawa waweze kujitawala wenyewe kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Mambo amechorwa kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Mwajuma ambaye wanafanya Ukahaba nyumbani kwa mpenzi wake. Kutokana na hali hiyo Mambo yuko tayari kumsaidia mpenzi wake kwa lolote wakati wa shida na raha ili aweze kupata haja yake.

Riwaya hii inamchora Mambo kama mwakilishi wa wanaume kama yeye ambao wapo katika jamii yetu (Masebo & Nyangwine, 2003). Wanaume hao wanawapenda wanawake kwa ajili ya kuwatekelezea matamanio yao ya kimwili na kuwasaidia pale inapobidi ili waweze kuendelea kupata haja zao.

4.4.3 Mtazamo wa Mwandishi kuhusu Ukahaba

Katika kuhakiki Riwaya ya *Vuta N'kuvute* tumeona kuwa mwandishi Shafi Adam Shafi amemchora Yasmin kama mhusika kahaba baada ya kufanya mapenzi na Denge. Sababu ya kufanya mapenzi na Denge si kwa tamaa ya kupata chochote kutoka kwa Denge, bali ni kwa ajili ya starehe na kumridhisha mpenzi wake (uk.145).

Baada ya Yasmin kujifungua alimpeleka mtoto shamba - Chaani ili akapewe jina kama ulivyokuwa utamaduni wao. Mtoto huyo alipewa jina na kuitwa Dhahir. Aliporudi toka safarini na kupewa taarifa kwamba Yasmin amejifungua mtoto, Denge alishtuka na kubakia akishangaa. Ingawa alifurahi kupata mtoto, lakini hakuwa tayari kumwoa Yasmin wala hakumsaidia kwa lolote katika malezi ya mtoto wao. (uk.182). Freud (1974) anaeleza kwamba wanawake au wanaume wengi wanaojishirikisha katika Ukahaba ni wale ambao wana uchu zaidi wa mapenzi na hivyo kushindwa kuwahudumia wapenzi wao wakati wa shida mfano mzuri tunamuona Denge kama ilivyoelezwa.

Hata hivyo, mwandishi hakutoa suluhisho bayana kuhusu suala la Ukahaba katika riwaya hii. Wasomaji hawapati mafunzo muafaka kuhusu suala hili kwani mwandishi halichambui kwa undani na kuonesha kwa kina athari za Ukahaba kwa wahusika, jamii na taifa kwa ujumla; ijapokuwa ni dhahiri kuwa kisaikolojia lazima Yasmin aliathirika sana kwani anaachiwa majukumu ya malezi akiwa mzazi pekee. Hata hivyo, inaelekea kuwa lengo la mwandishi huyu halikuwa hasa kuzionesha kwa undani athari hizo za Ukahaba, bali ni kusisitiza masaibu wanayokutana nayo wanamapinduzi kama Denge ambaye, zaidi ya kupigania haki za kijamii, pia anaoneshwa kama mtu wa kawaida mwenye hisia za mapenzi kama watu wengine (uk.145).

Ijapokuwa riwaya hii inasisitiza kuhusu umuhimu wa kuleta mabadiliko na hata mapinduzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii (pamoja na utamaduni) huko Zanzibar, uzito unawekwa zaidi katika siasa na uchumi, na ndiyo maana suala la kiutamaduni la mapenzi na Ukahaba linaelekea kufifishwa na hayo mengine (Mlacha, 1984).

Hata hivyo, mwandishi anajaribu kujadili ukombozi wa kiutamaduni ambapo anaonesha baadhi ya mila na desturi za Waswahili zinazomkandamiza mwanamke. Baadhi ya mila na desturi hizo ni ile ya kumlazimisha msichana kuolewa na mtu asiyemtaka kama walivyofanya wazazi wa Yasmin kwa kumwozesha Raza kwa nguvu (Ameir, 1988). Pia mwandishi anaonesha kuwa kuna mila ya kumweka mwanamke utawani, kama alivyofanya Shihab baada ya kumwoa Yasmin. Sanjari na hayo, mwandishi anaonesha kuwa kuna suala la utabaka na rangi katika jamii ya Waswahili (wa Unguja) kama mwandishi anavyoonesha makundi ya kijamii ya Wazungu, Wahindi, Wangazija, Waafrika, n.k (Shafi, 1999:130). Suala la ubaguzi wa rangi linajitokeza pale mwandishi anapowaonesha Wahindi wakikataa kuchanganyika na Waafrika kutokana na rangi zao.

Hivyo, mwandishi anaonesha kuwa mila na desturi hizi hazifai katika jamii kwani ni kikwazo kwa maendeleo ya mwanamke kijamii na kiutamaduni. Kwa hivyo, mwandishi anaishauri jamii kuwa, ili iweze kujikomboa kiutamaduni haina budi kuachana na mila na desturi zilizopitwa na wakati ambazo zinamnyanyasa mwanamke. Kwani mila na desturi hizo zinarudisha nyuma maendeleo ya mwanamke na jamii. Kwa ujumla, mwandishi amejibidiisha kuzingatia nadharia ya uhalisia katika kazi yake kwani ameweza kuichora jamii na kuelezea changamoto za maisha ya kikahaba katika jamii ingawa hakuweka bayana madhara ya ukahaba huo.

4.5 Uchambuzi wa Riwaya ya *Tata za Asumini*

Mhusika mkuu Asumini katika riwaya hii ni mwanafunzi katika chuo kikuu. Amelelewa kwenye mazingira magumu ambayo yanamfanya ashindwe hata kushirikiana na wanafunzi wengine anapofika chuo kikuu. Hatimaye Asumini anashindwa kuendelea na masomo yake kwa sababu ya tata zilizomo akilini mwake.

Anashindwa kuchagua kati ya maisha ya kisasa na yale ya kizamani jinsi alivyousiwa na wazazi wake. Kabla ya kuhama chuoni anamwandikia barua Maimuna waliyekuwa wakiishi pamoja na kumwambia kwamba ameamua kuhama chuoni na masomo yake kukomea hapo.

Anapohama kutoka chuo kikuu, Asumini haendi moja kwa moja hadi nyumbani kwao bali anakutana na Zaina ambaye wanaishi pamoja hadi pale Asumini anapokuwa na ugonjwa wa akili, akapelekwa hospitalini. Anamwandikia mchumba wake Sewa barua na kumwambia vile ulimwcngu ulivyomdhulumu yeye miongoni mwa watu wengine wengi. Katika barua hiyo hiyo, Asumini analalamikia malezi aliyopewa na wazazi wake ambayo yalimfanya ateseke kisaikolojia maishani mwake. Pia katika barua hiyo anamshauri Sewa asiwalee watoto wake wa kike jinsi yeye Asumini alivyolelewa na wazazi wake.

4.5.1 Usawiri wa Ukahaba katika *Tata za Asumini*

Mwandishi Said Ahmed Mohamed katika riwaya ya *Tata za Asumini* ameusawiri Ukahaba kwa namna tofauti. Mwandishi huyu amewachora baadhi ya wahusika wakijihusisha na Ukahaba kutokana na sababu mbalimbali. Anawaonyesha jinsi wanafunzi wa elimu ya juu wanavyojishirikisha na Ukahaba kutokana na tamaa ya kipato. Kwa mfano, katika ukurasa wa 48, mwandishi anamuonyesha Miriam akifanya mapenzi na Daddy ili aweze kujipatia fedha za kujikimu. Dondoo lifuatalo uk. 48 linafafanua:

> *"Baba'ako tajiri enh?" Aliuliza Asumini lakini Miriam alicheka kicheko cha kishetani, akijibu pasina kuwaza. "Ndio baba'angu*

huyu tajiri sana… utaelewa baadaye ubaba wake na utajiri wake, sasa hutayafahamu mambo haya".

Katika dondoo hilo mwandishi anamuonyesha Asumini akimuuliza Miriam kuhusu pesa nyingi anazopewa na Daddy. Miriam anafanya Ukahaba kwa ajili ya kupata pesa za kujikimu na kununulia mahitaji mengine.

Aidha, katika riwaya hii mwandishi anaonyesha kuwa suala la Ukahaba halipo kwenye vyuo vikuu tu, bali ni suala ambalo limo hadi ndani ya jamii. Mwandishi anamtumia Bi Time kuonyesha kuwa ndani ya jamii masuala ya Ukahaba yameenea. Wanajamii wanaendeleza Ukahaba katika rika mbalimbali kama vile vijana kwa vijana, watu wazima kwa watu wazima na hata watu wazima kwa vijana. Mwandishi anamtumia mhusika Bi Time uk.80 kueleza yafuatayo:

"Mwanzo niliogopa nikadhani ni mwambie mama kwani baba wakati huu nd'o alishakufa… lakini zile shilingi kumi nilizopewa na Mzee Omari nilimwachia mama yangu kwani kazi yake ya kuuza uji haikumpatia hata shilingi kumi kutwa.

Katika dondoo hilo mwandishi anamuonyesha Bi Time akisimulia namna anavyopata pesa za kumsaidia mama yake kutoka kwa Mzee Omari. Mzee huyu aliishi jirani na akina Bi Time wakati huo Bi Time ni mtoto lakini Mzee Omari hakujali ujirani wala ukaribu wake na mzazi wa Bi Time badala yake alikuwa akimpa pesa Bi Time ili aweze kufanya naye mapenzi.

Sambamba na hayo, mwandishi anaonyesha kuwa Ukahaba umo hadi kwa watu wa dini. Mwandishi anamtumia Bi Feruzi kuonyesha wanawake wanaofanya Ukahaba na watu wa dini. Dondoo lifuatalo uk. 81 linafafanua:

“Na miye si n’naye huyo mchuchu haja, Shehe wangu. Mambo yanapofikia upeo utamsikia akilalama ati anajuta kwa nini… hee-he, toba ya nini mtu kujinyima maji na huku kiu inamtilifu?

Kupitia dondoo hilo mwandishi anatuthibitisha namna ambavyo watu wa dini wanajihusisha na Ukahaba katika jamii. Mwandishi amemtumia shehe wa Bi Feruzi kama kiwakilishi cha viongozi wa dini ambao wanajihusisha na Ukahaba katika jamii.

Kwa ujumla mwandishi, Said Ahmed Mohamed katika riwaya ya *Tata za Asumini* ameusawiri Ukahaba kama suala ambalo ni gumu na zito kuzuilika katika jamii. Kwa sababu katika jamii ya leo Ukahaba unajitokeza katika nyanja mbalimbali za maisha. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, inadai kuwa matatizo yote ya kijamii yaelezwe bila kufichwa, kama ambavyo mwandishi ameusawiri Ukahaba katika jamii, kwenye taasisi za dini, mashuleni, vyuoni na kadhalika. Hivyo tunaona namna nadharia hii inavyodhihirika na kuchangia uchambuzi wa masuala ya kijamii kama yalivyo na bila kificho.

4.5.2 Wahusika Wanaojishughulisha na Ukahaba

Katika riwaya ya *Tata za Asumini*, mwandishi amewasawiri baadhi ya wahusika wake wakijihusisha na suala la Ukahaba kwa namna mbalimbali. Katika riwaya hii wahusika ambao wanahusishwa na Ukahaba ni kama vile Zaina, Daddy, Masika, Mwatima, Sewe, Mzee Omari na Miriam. Katika sehemu itakayofuata tutaelezea wasifu wa wahusika watano ili wawe wawakilishi wa wengine. Tuangalie wasifu wa wahusika Miriam, Zaina, Daddy na Sewa katika sehemu zitakazofuata.

4.5.2.1 Miriam

Miriam ni muhusika katika riwaya ya *Tata za Asumini* ambaye amechorwa kama mwanamke mrembo anayesoma chuo kikuu na kuishi katika bweni za chuo hicho. Licha ya pesa za kujikimu anazopewa na wazazi wake anategemea Ukahaba kupata pesa zaidi za kujikimu na kuendesha maisha yake katika bweni za chuo kikuu. Miriam ameoneshwa kuwa na mahusiano ya kingono na Daddy ambapo Miriam anamwita Daddy baba lakini anafanya naye mapenzi. Dondoo lifuatalo uk. 48 linafafanua:

> *"Ya ilahi." aliwaza Asumini …mtu huwa ana baba wangapi? Bila shaka Asumini alibaini toka mwanzo uwezo wa fedha aliokuwa nao Miriam tokea siku ya mwanzo Asumini alipoingia mle chumbani mwao. Viatu, kanzu, mapambo, mafuta, vinywaji… mradi jumla ya vitu vilivyothibitisha uwezo wake.*

Katika dondoo hilo mwandishi anamuonyesha Asumini akishangaa kuhusu Miriam anavyopata pesa nyingi kutoka kwa Daddy ambaye anamwita baba ingawa watu wanajua kama sio baba yake.

Kuhusu wasifu wa ndani, Miriam amechorwa kama ni msichana aliyekutana na maisha ya kawaida yasiyo rahisi wala magumu. Anasoma tokea shule ya msingi hadi chuo kikuu kwa uwezo wa wazazi wake. Miriam amechorwa kama ni msichana mwenye roho ya imani na huruma kwa sababu alikuwa wanasaidia sana rafiki zake mle chumbani mwao. Zaidi hayo, Miriam anaonekana kuwa na roho mzuri na moyo wa huruma kwa Asumini. Amekuwa akimsaidia rafiki yake huyu kwa hali na mali pale chumbani pao.

4.5.2.2 Zaina

Zaina ni muhusika katika riwaya ya *Tata za Asumini* ambaye amechorwa kama mwanamke mrembo ambaye anafanya kazi ya utopasi ya kufagia barabarani. Zaina amechorwa kuwa ni mwanamke chakaramu au chanja ambaye anaonekana kuwa na furaha muda wote.

Kuhusu wasifu wa ndani, Zaina amechorwa kama ni mwanamke anayeishi maisha ya kawaida yasiyo rahisi wala magumu. Anaishi mjini kwa kufanya kazi ya utopasi. Pia, Zaina amechorwa kama ni mwanamke mwenye roho ya imani na huruma kwa sababu alikuwa anamsaidia sana rafiki yake Asumini. Zaina anampokea rafiki yake Asumini na kuamua kuishi naye pale mjini baada ya Asumini kuhama chuo kikuu, Kila mara Zaina anaonekana kumsikiliza rafiki yake juu ya mambo anayotaka kufanyiwa. Kwa mfano, Zaina baadhi ya siku hutoroka kazini kwenda sokoni kununua vitu ambavyo Asumini ameagiza uk. 65.

4.5.2.3 Daddy

Daddy ni mhusika katika riwaya hii ya *Tata za Asumini* ambaye amechorwa kwa kuonyeshwa kuwa ni mtu mzima wa makamo mwenye uwezo kifedha. Daddy ni mpenda starehe na kubadilisha wasichana ambao anatembea nao kingono. Anatumia fedha alizonazo kuwahadaa wasichana kwa kuwapa fedha hizo au kuwanunulia vitu mbalimbali vya thamani kama vile nguo, mapambo, mafuta na kadhalika ili aweze kutembea nao kingono.

Daddy ameonyeshwa kuwa na mahusiano ya kingono na wasichana mbalimbali kwa mfano, katika ukurasa wa 53 mwandishi anamuonyesha Daddy akiwa na mpenzi

wake Miriam. Katika kuonyesha mahusiano yake na wasichana mbalimbali uk. 94 mwandishi anafafanua:

> *Kwa mbali Daddy alikuwa anamkumbuka msichana wa mwanzo aliyekwenda naye. Alimwona alivyomchukua katika njia ya burudani. Lakini msichana yule hakufua dafu kwa Asumini. Kasha alimkumbuka mwingine na mwingine na mwingine hata alishindwa kuwahesabu na wote hao Daddy alikiri kuwa hawakufua dafu kwa Asumini.*

Pia Daddy huyo huyo anaoneshwa akitumia uwezo wake kutaka kuanzisha mahusiano ya kingono na Asumini. Katika uk. 94, Daddy anamuuliza Asumini anataka kitu gani ili amnunulie na waendelee kuwa na mahusiano ya kingono. Kwa hakika Daddy ni kiwakilishi cha wanaume waovu wengi sana ambao wamo kwenye jamii zetu ambao wanatumia uwezo wao wa kifedha kuwaingiza wasichana wadogo katika Ukahaba. Kwa ujumla, watu kama Daddy hawafai kuigwa katika jamii zetu na wanapaswa kulaaniwa na kupigwa vita kwa kila hali.

4.5.2.5 Sewa

Sewa ni mhusika wa kiume katika riwaya ya *Tata za Asumini* ambaye ameonyeshwa kuwa ni kijana barubaru mwenye uwezo kiasi. Mhusika huyu anapenda starehe na kubadilisha wasichana kwa kutembea nao kingono. Anatumia fedha alizonazo kuwahadaa wasichana kwa kuwapa pesa au hata kuwanunulia vitu vya thamani kama vile nguo, mapambo, mafuta na wakati mwingine vyakula na vinywaji ili aweze kutembea nao kingono.

Aidha, Sewa anaoneshwa akitumia uwezo wake kutaka kuanzisha mahusiano ya kingono na Asumini. Katika uk. 53, ambapo anamualika Asumini kwenda nyumbani kwake. Asumini akiwa nyumbani kwa Sewa anaulizwa anataka andaliwe kitu gani. Mwandishi anamuonesha Sewa akiandaa chai na kuiweka katika buli kwa ajili ya Asumini. Kumwandalia Asumini chai na kumpa zawadi mbalimbali ni ishara ya ulaghai ili aweze kumpata Asumini wawe na mahusiano ya kingono. Kwa hakika Sewa ni kiwakilishi cha baadhi ya wavulana waovu ambao wamo ndani ya jamii yetu. Wavulana kama hawa wanatumia uwezo wao wa kifedha kuwaingiza wasichana wadogo katika Ukahaba. Kwa hakika, wavulana kama Sewa hawafai kuigwa katika jamii na inafaa kulaaniwa na kuchukuliwa hatua za kisheria kila wanapogunduliwa wakifanya hivyo katika jamii.

4.5.3 Mtazamo wa Mwandishi kuhusu Ukahaba

Katika kuhakiki Riwaya ya *Tata za Asumini* tumeona kuwa mwandishi Said Ahmed Mohamed amemchora Asumini kama mhusika alipata maisha magumu kutokana na harakati za maisha alizokutana nazo katika hosteli za chuo kikuu.

Mwandishi anamuelezea Asumini kama mwanagenzi wa dunia chafu na ngumu kwa yale aliyoyaona yanafanywa na wanawake wa hosteli za chuo kikuu. Katika riwaya hii mwandishi anawachora wasichana kama vile Zaina, Masika, Mwatima, Bitime, na Bimboga kama makahaba. Baadhi ya wahusika hawa wanafanya Ukahaba ili kujipatia huduma za kujikimu.

Hata hivyo, mwandishi hakutoa suluhisho bayana kuhusu suala la Ukahaba. Wasomaji hawapati mafunzo muafaka kuhusu suala hili kwani mwandishi halichambui kwa undani na kuonesha kwa kina athari za Ukahaba kwa wahusika,

jamii na taifa kwa ujumla; ijapokuwa ni dhahiri kuwa kisaikolojia lazima Asumini aliathirika sana kwani anapata na misukosuko na mivutano ya maisha na mapenzi kutoka kwa wanaume mbalimbali waliompenda kufanya naye Ukahaba. Hata hivyo, inaelekea kuwa lengo la mwandishi huyu halikuwa hasa kuzionesha kwa undani athari hizo za Ukahaba, bali ni kusisitiza masaibu wanayokutana nayo wasichana wanaotoka vijijini kwenda kusoma vyuo vikuu mijini. Kutokana na nadharia ya Saikolojia, tunaona kuwa wanadamu wengi hujiingiza katika masuala ya ngono kutokana na matamanio ya mwili na pia malezi ya kifamilia ambayo humsababishia mtu matatizo ya kisaikolojia hadi kujihusisha katika masuala ya uasherati.

Ingawa riwaya hii inasisitiza kuhusu umuhimu wa kuleta mabadiliko ya utamaduni katika jamii ya Watanzania, uzito unawekwa zaidi katika masuala ya malezi ya wasichana maana suala la kiutamaduni la mapenzi na Ukahaba linaelekea kufifishwa na hayo mengine.

Hata hivyo, mwandishi anajaribu kujadili ukombozi wa kiutamaduni ambapo anaonesha baadhi ya mila na desturi za Waswahili zinazomkandamiza mwanamke. Baadhi ya mila na desturi hizo ni ile ya kumnyima uhuru msichana kiasi cha kumuathiri kisaikolojia.

Hivyo, mwandishi anaonesha kuwa mila na desturi hizi hazifai katika jamii kwani ni kikwazo cha maendeleo ya mwanamke kijamii na kiutamaduni. Kwa jumla, uchambuzi wetu kuhusu mwandishi umezingatia nadharia za uhalisia na saikolojia ambazo tumezitumia kama mwongozo wa utafiti huu. Nadharia hizi zimetusaidia kubaini hali halisi za maisha jamii zinavyoonekana katika jamii na namna matatizo ya kisaikolojia yanavyowaathiri wanajamii hiyo.

4.6 Sababu za Ukahaba katika Riwaya na Jamii

Sehemu hii inajadili na kufafanua lengo mahususi la pili ambalo lilitaka kubainisha sababu za Ukahaba katika riwaya na jamii. Kwa mujibu wa utafiti huu, inaonekana kuwa katika jamii kuna watu wengi ambao wanalipinga suala la Ukahaba. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kufanya Ukahaba ni tendo la aibu na fedheha linalolaaniwa na watu wa imani za dini mbalimbali. Hivyo, mwanamke anayejishughulisha na Ukahaba anaonekana kama aliyekosa malezi na maadili mema katika familia yake.

Kwa kutumia mbinu za usaili, hojaji na mahojiano ya kikundi, utafiti huu ulibaini sababu kadhaa. Uchambuzi wa sababu hizi umeongozwa na nadharia za uhalisia na saikolojia ambazo tumeziteua kuzitumia katika utafiti huu. Hivyo, wahojiwa wetu walitaja sababu kama ifuatavyo hapa chini:-

Kwanza, tamaa ya kipato au hadhi. Kuna baadhi ya wanawake wanafanya mapenzi na wanaume wasio waume zao ambao wana uwezo kifedha kwa tamaa ya kupata mali kama vile kujengewa nyumba, kununuliwa magari na mengineyo. Pia baadhi ya wanawake hufanya mapenzi ili waweze kupandishwa vyeo kazini na wengine kupata ufaulu wa daraja la juu masomoni. Sababu hii inabainishwa kupitia mhusika Miriam na wenzake katika riwaya ya *Tata za Asumini* uk. 53.

Pili, kuna baadhi ya wanawake ambao hufanya Ukahaba na wanaume wasio waume zao kwa tamaa ya kuolewa. Kuna baadhi ya wanaume ambao huwahadaa wanawake kwa kuwataka watembee nao kwanza ndio baadae waweze kufunga nao ndoa. Katika hali kama hiyo kuna wanaokubali na hatimaye wanajikuta wametumbukia katika dimbwi la Ukahaba. Sababu kama hii pia tunaibaini katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*

ambapo Yasmin anafanya Ukahaba na Denge kwa kutaraji kuolewa. Aidha, katika riwaya ya *Tata za Asumini* tunamuona Asumini akimuomba Sewa amuoe, uk. 54

Tatu, kuna wanawake ambao hujiingiza katika Ukahaba kwa ajili ya kujistarehesha tu. Hapa kuna wanawake wa aina mbili; kuna wale wanawake wasio na waume na wanahamu kufanya ngono. Pia kuna wanawake wenye waume na wanatamani kufanya mapenzi wanaume wa nje ya ndoa. Hawa ni wanawake ambao wanajihisi kutotosheka kimapenzi kwa waume zao wa ndoa. Sababu hii haikuoneshwa kwa upande wa wahusika wanawake katika riwaya teule zote mbili. Bali kwa upande wa wanaume takriban wote wanafanya Ukahaba kwa lengo la kutuliza kiu ya miili yao. Hayo tunayaona kupitia wahusika kama vile Denge na Mambo wa *Vuta Nkuvute* na Daddy, Mzee Omari na Sewa katika riwaya ya *Tata za Asumini.*

Nne, kuna wanawake ambao huifanya biashara miili yao kwa kufanya Ukahaba na watu wasio waume zao kwa ajili ya kupata mahitaji yao ya kila siku. Hawa ni wale wanawake maskini ambao huitumia miili yao kama vitega uchumi vya kujipatia mahitaji muhimu kama vile, chakula, nguo na malazi. Baadhi ya wanawake wa kundi hili hujikuta wanafanya Ukahaba katika maisha yao ya kila siku. Sababu hiyo inabainishwa katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kupitia mhusika Mwajuma na katika riwaya ya *Tata za Asumini* inabainishwa kupitia wahusika Miriam, Zaina, Bi Time, Bi Feruzi , Masika na Mwatima.

Tano, kuna wanawake ambao wapo katika ndoa ambao hutoka nje ya ndoa zao kwa kutembea na wanaume wasio waume zao kwa ajili ya kupata watoto. Hawa ni wale wanawake wanaogundua kwamba waume zao wa ndoa wana matatizo ya mfumo wa uzazi kiasi ambacho hawana uwezo wa kuzaa. Hivyo wanawake hao hutoka nje ya

ndoa zao kutafuta watoto. Sababu hii haikujibainisha katika riwaya teule zote mbili ambazo zimetumika katika utafiti huu. Hata hivyo, wanajamii waliitaja kama sababu mojawapo inayowapeleka wanawake kutoka nje ya ndoa na hatimaye kutumbukia katika dimbwi la Ukahaba.

Sita, kuna wanawake ambao hujiingiza katika Ukahaba baada ya kubakwa. Hawa ni wale wanawake ambao hulazimishwa kufanya ngono kwa nguvu au bila ridhaa zao. Miongoni mwa sababu za kubakwa zilizobainishwa ni pamoja na kuwa na sura nzuri, kutembea nusu uchi na kukataa kulipa fadhila kwa wanaume waliowasaidia jambo fulani. Sababu hii pia haikujibainisha katika riwaya teule zote mbili ambazo zimetumika katika utafiti huu. Ingawa, wanajamii waliitaja kama sababu mojawapo inayowapeleka wanawake kutumbukia katika dimbwi la Ukahaba. Katika ufafanuzi wao walieleza kuwa mwanamke baada ya kubakwa mara nyingi huathirika kisaikolojia, hivyo kujishirikisha katika Ukahaba kwao huona kama suala la kawaida kwa sababu hofu huwa imeshawaondoka.

Sababu tulizozibainisha na kuzieleza hapo juu ni miongoni mwa mambo yaliyobainishwa na watoa taarifa wetu kuwa yanawaingiza wanawake katika kufanya Ukahaba. Kwa sababu hizo, baadhi ya wanawake hujikuta wakibeba mimba za nje ya ndoa bila kutarajia ambapo baada ya kubeba mimba hizo hukumbana na matatizo mbalimbali kama vile ya kimwili, kijamii na ya kiuchumi.

Tukiziangalia sababu hizi na kuzilinganisha na yanayotokea katika riwaya mbili tulizozichambua itaonekana kuwa baadhi ya sababu zimejitokeza katika riwaya na nyingine hazikujitokeza. Kwa mfano, wahusika wakuu wa riwaya zote mbili; Asumini wa *Tata za Asumini* na Yasmin wa *Vuta N'kuvute,* wahusika hawa

walifanya mapenzi kutokana na sababu ya tatu hapo juu. Mfano, Asumini alifanya mapenzi na Dadi ili kujistarehesha mwili wake (Mohamed, 1990). Aidha, Yasmin alikuwa akifanya mapenzi na Denge kwa lengo la kujistarehesha (Shafi, 1999). Kwa upande mwingine, katika *Tata za Asumini* tunaoneshwa Asumini akifanya mapenzi na Dadi kwa hali ya kulazimishwa. Hali hii tunaweza kuiweka katika sababu ya sita hapo juu.

Pia, kuna wahusika Zaina, Mwatima, Bi Time, Bi Mboga na wengineo katika riwaya ya *Tata za Asumini* na Mwajuma wa riwaya ya *Vuta N'kuvute,* wahusika hawa wanaoneka kufanya Ukahaba kulingana na sababu ya nne hapo juu. Japokuwa wahusika hawa hawakuoneshwa kupata athari, lakini ni miongoni mwa wanawake wanaouza miili yao ili waweze kujipatia mahitaji yao ya kila siku kama inavyooneshwa na wanajamii.

Kwa mujibu wa utafiti huu sababu ya kwanza, ya pili na ya tano zilizobainishwa na data ya wanajamii, sababu hizi hazikujitokeza katika riwaya hizi. Hivyo, tunaweza kusema kuwa waandishi wa riwaya hizi hawakulipa uzito unaostahili suala la Ukahaba. Pengine waliliona halina athari kubwa katika jamii yao likilinganishwa na suala la harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya. Kwa ujumla, nadharia za uhalisia na saikolojia zimetusaidia kuchambua sababu za Ukahaba zilizobainishwa katika riwaya teule na zili zilizobainishwa na watoa taarifa wetu wakati wa ukusanyaji wa data za uwandani.

4.7 Athari za Ukahaba

Katika sehemu hii tutajadili lengo mahususi la tatu ambalo lilikuwa ni kuonyesha athari za Ukahaba kwa wahusika na jamii kwa ujumla. Data za sehemu hii zilikusanywa kwa mbinu za usaili, hojaji na majadiliano ya kikundi. Uchambuzi wa data umefanywa kwa kutumia nadharia za uhalisia na saikochanganuzi. Utafiti umebaini kuwa kuna athari chanya na hasi zinazotokana na Ukahaba. Mfano wa athari chanya za Ukahaba ni wahusika kupata kutuliza matamanio ya nafsi zao na wanawake kupata mahitaji wanayoyataka kutoka kwa wateja wao. Katika sehemu zinazofuata hebu tuangalie kwa kina athari hasi za Ukahaba

4.7.1 Athari kwa Wahusika

Katika kipengele hiki tumeeleza na kujadili athari za Ukahaba kwa wahusika. Athari hizo kwanza tutazichunguza kwa wahusika wanawake, pili kwa wahusika wanaume, tatu athari za Ukahaba kwa jamii na taifa kwa jumla. Tuzingatie maelezo na mjadala hapa chini:

4.7.1.1 Athari kwa Wahusika Wanawake

Uchunguzi huu umebaini kuwa kuna matatizo kadhaa yanayowapata wanawake wanaojishughulisha na Ukahaba. Kwa kweli matatizo haya hukwamisha ustawi na maendeleo yao katika nyanja mbalimbali za maisha. Miongoni mwa matatizo yaliyobainishwa katika utafiti ni haya yafuatayo:

Kwanza, kutengwa na familia zao. Hili ni tatizo ambalo limewakumba wanawake waliobeba mimba za nje ya ndoa katika baadhi ya familia. Kuna baadhi ya wazazi wenye misimamo mikali ambao huwafukuza watoto wao wakike wanaobeba mimba za nje ya ndoa. Wazazi huchukulia kuwa mtoto wao amevunja maadili ya jamii na

kutia aibu familia yao. Kwa hivyo huchukua hatua ya kumfukuza nyumbani jambo ambalo hupelekea kukosa huduma bora za afya na matunzo.

Pili, kufukuzwa kazi au kuachishwa masomo. Baadhi ya wanawake na wasichana wanaofanya Ukahaba wakiwa ni wafanyakazi au wanafunzi hukumbwa na tatizo la kufukuzwa au kuachishwa kazi na waajiri wao. Sambamba na hilo, wanawake ambao bado ni wanafunzi hasa katika ngazi za msingi na sekondari nao pia hukumbwa na tatizo hili. Shule na taasisi nyingine za elimu huwafukuza masomo wanafunzi wakike ambao wamegundulika wakifanya Ukahaba. Suala hili linafanywa bila kujali haki za msingi za kupata elimu ambapo wanawake waliofukuzwa masomo hukosa haki yao ya kupata elimu.

Tatu, kukanwa na kutelekezwa na wanaume zao. Jamii imebainisha kuwa baadhi ya wanawake wanaofanya Ukahaba hukataliwa na wapenzi wao na pengine kutelekezwa kabisa. Mara nyingi wanaume huwakataa wapenzi wao wa kike mara tu wanapobeba mimba. Wanaume kama hao hukata mawasiliano na wapenzi wao bila kupeleka huduma yoyote ya kumsaidia mjamzito. Jambo ambalo hupelekea mwanamke kukosa huduma bora za kujikimu na matunzo ya mtoto.

Nne, kuachwa na waume zao wa ndoa. Tatizo hili huwakumba wanawake walio katika ndoa ambao hufanya Ukahaba kwa sababu tulizokwisha zieleza hapo awali. Wanaume wengi wanapogundua kwamba wake zao ni makahaba basi hufikia uamuzi wa kuachana nao. Kuna matatizo kadhaa ambayo yanaweza kujitokeza kwa mwanamke baada ya kuachwa na mume wake wa ndoa hasa katika kipindi cha ujauzito. Baadhi yao hupata maisha magumu na usumbufu wa kisaikolojia.

Tano, baadhi ya wanawake wanapojigundua kuwa wameshabeba mimba huchukua uamuzi wa kuzitoa mimba hizo. Kama inavyoeleweka kuwa kutoa mimba si jambo la mzaha hata kidogo, wanawake wengi wanaotoa mimba hupoteza damu nyingi na wengine huharibu kabisa vizazi. Jambo hili husababisha vifo kwa baadhi ya wanawake.

Sita, kuna wanawake ambao hujinyonga mara tu wanapojigundua wamepata ujauzito au maambukizi ya UKIMWI. Kutokana na kuwa suala hili ni la aibu katika jamii, baadhi ya wanawake wanafikia uamuzi huo wa kupoteza maisha yao ili kukwepa lawama na karaha za jamii. Jambo hili la kujinyonga kwa kitanzi au kunywa sumu hutokea mara kadhaa katika jamii zetu.

Saba, baadhi ya wanawake makahaba wanapobeba mimba za nje ya ndoa hulea mimba lakini huchukua hatua ya kuwatupa au kuwaua watoto waliojifungua. Katika jamii yetu ya leo suala la kuonekana mtoto mchanga ametupwa akiwa hai au amekwisha kufa ni jambo lisiloshangaza. Wanawake wanaotupa au kuua watoto hupata matatizo mbalimbali wakati wanapojulikana. Matatizo hayo ni kama vile kulaaniwa na jamii, kushitakiwa na kufunguliwa kesi mahakamani ambapo hatimaye huishia katika kifungo cha jela.

Hayo ni baadhi ya matatizo yanayowakabili wanawake wanaobeba mimba za nje ya ndoa katika jamii zetu. Kwa ujumla matatizo hayo hupelekea wanawake hao kuathirika kisaikolojia, kupoteza mwelekeo wa maisha kwa kuishi maisha duni kutokana na kukosa ushirikiano mwema na jamii. Kwa majumuisho kutoka katika maelezo yaliyotangulia, tunaweza kueleza kuwa, madhara makubwa yanayotokana

na ujihusishaji katika masuala ya ukahaba ni Mimba zisizotarajiwa na Magonjwa ya zinaa hasa UKIMWI.

Hata hivyo, tukiyazingatia kwa kina matatizo hayo na kuyalinganisha katika riwaya tumeona kuwa matatizo takribani yote hayakubainishwa vilivyo katika riwaya teule. Hivyo tunaweza kusema kuwa waandishi wa riwaya hizi wamekwepa uhalisia wa kulibainisha suala la Ukahaba na matatizo yatokanayo na suala hilo.

4.7.1.2 Athari kwa Wahusika Wanaume

Matatizo ya Ukahaba hayawapati wanawake peke yao, pia kuna baadhi ya matatizo ambayo huwakabili wanaume wanaojihusisha na Ukahaba katika jamii zao. Baadhi ya matatizo yaliyobainishwa kuwa huwakumba wanaume ambayo yamebainishwa na wahojiwa wetu ni haya yafuatayo:

Kwa vile jamii hutofautiana kimila na kidesturi kutoka eneo moja hadi jingine, hivyo, katika baadhi ya maeneo wanaume makahaba hulazimishwa kuwaoa wasichana waliowapa mimba za nje ya ndoa. Wazazi wa mwanamke huwatafuta wazazi wa mwanaume na kushauriana ili kupata suluhisho la tatizo. Katika hali kama hiyo wazazi wa mwanamke hushikilia mtoto wao aolewe ili waondokane na aibu inayowakabili. Kulazimishwa kuoa ni tatizo kwa wanaume wale ambao hawajawa tayari kuoa kwani huwapangulia mipango yao ya kimaendeleo.

Pia, kuna baadhi ya wazazi wa wanawake waliopewa mimba ambao hulazimisha kuwa wanaume waliowapa mimba watoto wao walipe faini kufidia kosa walilofanya. Mwanaume anaweza kupigwa faini ya fedha taslimu au mali ya aina yoyote. Kulipa faini ni tatizo kwa wanaume wengi ambao wamo katika familia maskini. Kutokana na hali hiyo, mwanaume aliyeshindwa kulipa faini anaweza kushitakiwa

mahakamani na kufikia adhabu ya kifungo na kukosa kufanya shughuli za maendeleo.

Aidha, wakati mwingine tatizo la kufukuzwa shule haliwapati wanawake makahaba peke yao. Pia mwanafunzi wa kiume anayempa mimba mwanafunzi wa kike naye, hufukuzwa masomo na wengine huacha masomo wenyewe kwa kutoroka shule ili kukimbia tatizo lililojitokeza. Hali hii pia humfanya mwanafunzi wa kiume kukosa elimu na kupanguka kwa mpangilio mzima wa maisha yake.

Tukirejelea katika riwaya teule, tunabaini kuwa hakuna matatizo yaliyobainishwa yanayoweza kumpata mhusika mwanaume ambaye ni kahaba. Waandishi kwa kiasi fulani wamekengeuka uhalisia wa suala hili ikilinganishwa na mtazamo wa wanajamii. Kwa sababu kutokubainisha matatizo hayo kunaweza kuifanya hadhira ya waandishi kuliona suala hili kama suala jepesi lisilo na athari yoyote kwa jamii na kwa Taifa.

4.7.2 Athari kwa Jamii

Hapo nyuma tumeona matatizo yanayowapata wahusika wanawake na wanaume wanaohusika na mimba za nje ya ndoa. Ni dhahiri kwamba matatizo yanayowapata wanajamii yanaleta athari kwa jamii mzima na Taifa kwa ujumla. Kwa mujibu wa uchunguzi wetu Ukahaba husababisha matatizo mbalimbali kwa jamii na taifa kwa jumla. Baadhi ya matatizo ambayo yalibainishwa na watoa taarifa wetu katika majadiliano ya kikundi yalikuwa haya yafuatayo:

Kwanza, jamii kuvurugika kimaadili ni tatizo moja kubwa ambalo hujitokeza katika jamii ikiwa suala la Ukahaba limeshamiri katika jamii hiyo. Kwa hakika suala la Ukahaba linatokana na uzinzi. Kushamiri kwa vitendo hivi kunaleta matatizo kadhaa

yakiwemo kuongezeka umasikini, watoto kukosa malezi bora, heshima inapotea na mmomonyoko wa maadili unaongezeka katika jamii.

Pia, Ukahaba husababisha kushamiri kwa vitendo vya uhalifu. Tumekwishaeleza kuwa baadhi ya wahusika wanaume na wanawake husimamishwa masomo au kazi. Wote hawa wanahitaji fedha za kujikimu mahitaji yao ya lazima ya kila siku. Kwa vile wengi hawana msingi, huwabidi watumie njia yoyote kutafuta riziki. Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wahusika hujiingiza katika vitendo vya uhalifu kama vile wizi, utapeli, ujambazi wa kutumia nguvu na mengineyo.

Kuwa na watu wenye elimu ndogo ni tatizo jingine linalojitokeza katika jamii na Taifa litokanalo na Ukahaba. Mara nyingi wanawake makahaba wanaopata mimba za aina hii na hata wanaume wanaowapa mimba wakiwa bado wako shule huacha au huachishwa masomo baada ya kutokea kwa suala hili. Si watu wengi wenye uwezo wa kuwaendeleza watoto wao kielimu, hivyo watu hawa hukosa elimu na Taifa kukosa wataalamu wa fani mbalimbali.

Tatizo jingine ni kuongezeka kwa watoto wa mitaani. Kama tunavyojua kwamba Ukahaba husababisha kuongezeka watoto wa mitaani katika jamii. Watoto wengi wanaozaliwa nje ya ndoa huathirika kisaikolojia kutokana na kukosa matunzo, malezi na huduma bora za kiafya na kielimu. Watoto wengine huacha shule kutokana na kukosa hudumu za msingi na kujiingiza katika ajira za watoto, vitendo vya uhalifu kama vile wizi na unyang’anyi.

Pia tumeona kuwa baadhi ya wanawake wanapopata mimba za nje ya ndoa hufikia uamuzi wa kujinyonga na kupoteza maisha, baadhi ya wanaume hushitakiwa na kuhukumiwa kifungo cha muda mrefu jela. Jambo hili husababisha Taifa kupoteza

nguvu kazi kwani kama tunavyojua kwamba vijana ndio tegemeo la Taifa kiuzalishaji. Kutokana na hali hiyo, Taifa hupoteza rasilimali watu ambao wengine wanaweza kuwa wataalamu wa fani mbalimbali hapo baadaye.

Kutokana na matatizo hayo, umaskini huongezeka katika jamii kwa kuongezeka kwa wategemezi, watu waliopoteza dira na mwelekeo katika masuala ya kiuchumi na watu wanaoishi katika hali ya kukata tamaa. Hivyo Taifa kupata mzigo mkubwa unaohitaji kuhudumiwa katika kila hali. Jambo ambalo kwa asilimia kubwa huchangia Taifa kuwa na uchumi tegemezi.

Ingawa matatizo hayo hayakubainishwa na waandishi katika riwaya teule, ni vema tuelewe kuwa suala la Ukahaba lina athari kubwa kwa jamii. Waandishi wa kazi za fasihi hawana budi kulichunguza kwa kina suala hili ili waweze kuwasilisha kazi zao bila kukwepa uhalisi wake katika jamii.

4.8 Mtazamo wa Jamii kuhusu Ukahaba

Mitazamo ya jamii na sheria inatofautiana kati ya nchi na nchi. Hata kama Ukahaba unapatikana kote duniani umepigwa marufuku katika nchi nyingi. Lakini mahali pengine penye sheria dhidi ya Ukahaba polisi inafumba macho au kutofuatilia biashara hii.

Kwa kutumia mbinu ya usaili utafiti huu ulibaini mtazamo wa jamii ya Waswahili suala la Ukahaba kama ifuatayo:

Kwanza, Ukahaba hutazamiwa kama jinai. Watendaji wanatishiwa kwa adhabu za kisheria kuanzia faini, jela hadi adhabu ya mauti na kadhalika. Mara nyingi ni hasa makahaba wanaolengwa kwa adhabu hizi, lakini mahali pengine pia wateja. Hata

hivyo, katika nchi nyingi penye sheria dhidi ya Ukahaba vyombo vya dola vinafunga macho au kutofuatilia biashara hii.

Pili, Ukahaba hutazamiwa kama ubaya unaovunja heshima hasa ya wanawake yaani malaya. Malaya huangaliwa kama waathirika wanaostahili kusaidiwa kwa hiyo hawana adhabu. Lakini wote wengine wanaofaidika na Ukahaba wanalengwa kwa adhabu: wenye danguro, makuwadi, washiriki katika biashara ya makahaba hadi wateja wenyewe katika jamii.

Tatu, Ukahaba hutazamiwa kama ubaya usioshindikana kwa hiyo serikali imetunga za siri sheria na taratibu kwa lengo la upatikanaji wa Ukahaba. Kwa mfano, nymba za kulala wageni ndio danguro hivyo zinapaswa kusajiliwa na serikali, zinatembelewa na idara ya afya ya umma; malaya wanaruhusiwa katika mitaa maalumu ya miji pekee, wanapaswa kuangaliwa na matibabu mara kwa mara. Vijiji na miji midogo vinaweza kuzuia Ukahaba katika maeneo yao.

Nne, Ukahaba hautazamiwi tena kama jinai wala kosa bali kama chaguo la watu wazima. Kwa hiyo Ukahaba huangaliwa kama namna ya biashara kama biashara nyingine; malaya huitwa "wafanyakazi wa ngono" wanatakiwa kulipa kodi na wanalindwa na sheria za kazi. Hali hii inatokana na jamii zetu kuiga tamaduni za kigeni za Ulaya na Marekani.

Kwa hiyo, jamii ina mtizamo hasi kuhusu Ukahaba kutokana na misimamo ya imani za kidini lakini kutokana na sheria za serikali kuwazuia wanajamii kuchukua sheria mikononi mwao suala hili limebaki likiendelea bila kizuizi. Kwa ujumla, nadharia za uhalisia na saikolojia ambazo tuliziteuwa kama mwongozo wa utafiti huu zimetusaidia kugundua sababu na athari za Ukahaba katika jamii. Kama tulivyoona

hali halisi kuhusu Ukahaba katika jamii ni matokeo ya hali ya maisha na athari za kisaikolojia katika jamii.

4.9 Hitimisho

Katika sura hii, tuwasilisha na kuchambua data zilizokusanywa kutoka maktabani na uwandani. Pia tumebainisha suala la Ukahaba lilivyosawiriwa katika riwaya na uhalisia wake katika jamii, sababu za wahusika kujiingiza katika uhakaba na athari zake kwa wahusika na jamii kwa jumla na mwisho tukahitimisha.

SURA YA TANO

MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza muhtasari wa mjadala wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo ya mtafiti kuhusu utafiti zaidi. Aidha, ni sura itakayotoa tathmini ya utafiti kwa ujumla, kuanzia lengo kuu, malengo mahususi na maswali ya utafiti.

5.2 Muhtasari wa Mjadala wa Utafiti

Katika sehemu hii tutaelezea muhtasari wa mjadala kuanzia sura ya kwanza hadi sura ya tano. Kila sura imeanza kwa utangulizi na kuendelea na mjadala na kuishia na hitimisho la sura inayohusika. Hivyo basi, Tasnifu hii ina jumla ya sura tano zilizopangiliwa kulingana na taratibu za uandishi wa ripoti ya utafiti.

Sura ya kwanza ambayo ni utangulizi wa jumla inatoa maelezo ya awali yanahusu ufafanuzi wa mada ya utafiti pamoja na kueleza umuhimu wa utafiti huu. Sura hii imeanza kwa kueleza taarifa za awali za utafiti ambazo ni usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti pamoja na mpangilio wa Tasnifu.

Sura ya pili imeeleza mambo matatu ambayo ni mapitio ya kazi tangulizi, kiunzi cha nadharia ya utafiti pamoja pengo la utafiti. Katika mapitio ya kazi tangulizi, sura hii imefafanua kazi tangulizi mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti ambazo mtafiti alizipitia. Lengo kuu la kupitia kazi tangulizi hizo lilikuwa ni kubaini pengo la utafiti ikiwa ni pamoja na kupata mwanga wa masuala muhimu ya kufanya ili kufikia malengo ya utafiti.

Aidha, Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti ambapo imefafanua mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Kwa ujumla, sura hii imeeleza namna taarifa za utafiti huu zilivyokusanywa na kuchambuliwa hadi kuandikwa ripoti hii ya utafiti. Taarifa za utafiti zimekusanywa kwa mbinu kuu tatu za ukusanyaji wa data. Mbinu hizo ni majadiliano ya vikundi, usaili na hojaji. Pia sura hii imeeleza mbinu zilizotumika katika mchakato wa uteuzi wa sampuli na mbinu zilizotumika katika uchambuzi wa data za utafiti.

Halikadhalika, sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data. Kwa ujumla sura hii ndio kiini cha utafiti huu kwa sababu data zote zilizokusanywa maktabani na uwandani zimewasilishwa katika sehemu hii. Uchambuzi wa data za utafiti umefanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi wa kifasihi pamoja na mbinu ya kimaelezo. Kwa hakika sura hii inatoa matokeo ya utafiti mzima kuhusu dhamira ya Ukahaba katika riwaya ya Kiswahili.

Sura ya tano ambayo ndiyo ya mwisho inahusu muhtasari wa mjadala wa utafiti, hitimisho na mapendekezo. Hii ni sura ambayo inatoa muhtasari wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti na mapendekezo ya mtafiti baada ya kukamilisha utafiti ili kujenga taaluma ya fasihi kwa kufanyika utafiti zaidi.

5.2.1 Kujibu Maswali ya Utafiti

Katika mchakato wa kuchunguza na kujadili usawiri suala la Ukahaba katika Riwaya ya *Vuta N'kute* na *Tata za Asumini* pia utafiti huu ulijielekeza kujibu maswali ya utafiti ambayo msingi wake ni malengo mahususi ya utafiti huu. Maswali hayo yalikuwa matatu kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza liliuliza: *Kuna usawiri gani wa Ukahaba na wahusika makahaba katika Riwaya za Vuta N'Kuvute na Tata za Asumini?* Kama ambavyo imebainishwa, suala la Ukahaba limeonyeshwa katika riwaya hizi. Waandishi wengi wa riwaya, wakiwemo wa *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* wamewachora baadhi ya wahusika wakijihulisha na suala hili. Katika riwaya ya *Vuta Nkuvute*, kwa mfano, mwandishi amewabainisha wahusika kama vile; Yasmin, Denge, Mwajuma na Mambo kama wahusika wanaojishirikisha na Ukahaba. Aidha, katika riwaya ya *Tata za Asumini* mwandishi amewabainisha wahusika kama vile Asumini, Zaina, Masika, Mwatima, Bimboga na Dadi kama wahusika wanajihusishwa na vitendo vya Ukahaba.

Swali la pili la utafiti huu lilikuwa hivi: *Kuna uhalisia wa kiasi gani wa sababu za Ukahaba zinazojitokeza katika Riwaya za Vuta N'Kuvute na Tata za Asumini na katika jamii?* Kulingana na data yetu, tunaona kuwa suala la Ukahaba alijaibuliwa kwa kina katika kazi za fasihi. Kwa sababu kulingna na maadili, desturi, silika na kaida za jamii, suala hili ni suala la aibu kwa wahusika. Mwanamke kahaba huwa anaaibisha familia yake. Familia hiyo hupoteza heshima yake na kuonekana kuwa ni familia ya wahuni, waasherati, malaya na wala haina malezi na maadili mema.

Kwa upande wa sababu zinazowaingiza wavulana na wasichana katika Ukahaba, utafiti umebaini kuwa kuna sababu kadhaa ambazo zinachangia wahusika kujihusisha na Ukahaba katika jamii zao. Miongoni mwa sababu ambazo zimebainishwa na watoa taarifa wetu ni kama vile, umasikini, starehe, mazoea, kwenda na wakati, tamaa za kimwili na ukosefu wa malezi.

Kwa hiyo, katika hali halisi, jamii inalitazama suala la Ukahaba kama jambo hasi lisilo na faida kwa mhusika na jamii kwa ujumla. Suala hili halikubaliki na

linapingwa na dini za imani mbalimbali sambamba na mila na desturi za jamii inayohusika. Kwa upande wa riwaya teule tunaona kwamba waandishi wa riwaya zote mbili wanaonekana kubainisha kuwa sababu kuu ya wasichana kujiingiza katika Ukahaba kuwa ni umasikini na kustarehesha miili yao bila kuonyesha sababu nyingine kama vile za kisaikolojia ambazo zimebainishwa na watoa taarifa wetu.

Swali la tatu lilitaka kubainishiwa athari zifuatazo: *Kuna athari gani za Ukahaba zinazowapata wahusika na jamii kwa ujumla?* Matokeo ya utafiti huu yanabainisha kuwa mitazamo ya waandishi wa riwaya na ya jamii kuhusu suala la Ukahaba kwa kiasi fulani yanapingana. Katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* ambazo tumezichunguza, athari za Ukahaba hazikubainishwa waziwazi. Hii ina maana kuwa waandishi wamelichukulia kama ni suala jepesi linaloweza kujitokeza katika jamii ingawa halikubaliki lakini hawaoneshi kwa kina athari zake kwa wahusika na jamii kwa ujumla.

Kwa upande wa jamii, japokuwa suala la Ukahaba limeanza kuzoeleka, bado suala hili linapingwa kwa kiasi kikubwa sana kutokana na athari zake. Watoa taarifa wetu waliainisha kuwa Ukahaba una athari chanya na hasi kwa wahusika. Kwa upande wa athari chanya zilizobainishwa ni wahusika kukidhi matamanio ya nafsi zao na kupata pesa. Lakini athari hasi ni nyingi sana kwa mfano, wahusika wanaweza kupata magonjwa ya kuambukiza, kupata mimba zisizotarajiwa, kuonekana wahuni, na kadhalika. Kwa upande wa athari hasi kwa jamii zilizotajwa ni kuongeza kwa watoto wa nje ya ndoa, jamii kukosa nguvu kazi hasa pale wahusika wanapopata magonjwa, na jamii kupoteza heshima mbele ya jamii nyingine.

5.2.2 Mchango wa Utafiti

Kwa ujumla, utafiti huu una mchango mkubwa katika taaluma ya fasihi na utunzi wa riwaya za Kiswahili hususani kwa jamii ya Wazanzibari. Kwanza, unatoa mchango wa kubainisha usawiri wa suala la Ukahaba katika riwaya za Kiswahili na uhalisia wake katika jamii. Utafiti umeweza kuwaweka bayana wahusika wanaojihusisha na Ukahaba katika riwaya teule. Pili, utafiti huu umeweza kubainisha sababu zinazowafanya wavulana na wasichana kujihusisha na vitendo vya Ukahaba katika jamii na mtazamo wa jamii juu ya Ukahaba. Tatu, utafiti huu unachangia kuonyesha athari hasi za Ukahaba zinazoweza kujitokeza kwa wahusika wanaojishuhulisha na suala hili katika jamii na athari zinaweza kuikabili jamii kwa kuwemo wahusika wa Ukahaba katika jamii hiyo.

Zaidi ya hayo, utafiti huu umegundua kuwa kuna wanajamii walio wengi wanaamini kuwa kahaba ni mwanamke pekee. Hilo linathibitishwa na hoja za wahojiwa wetu walipodai kwamba mtendaji Ukahaba anayepokea malipo huitwa kahaba au malaya ambapo mshiriki anayetoa malipo huitwa mteja. Hapo watafitiwa wetu walilenga kuwa makahaba ni wanawake ambao wanaojiuza lakini mnunuzi ni mteja kama walivyo wateja wa biashara nyingine. Kuhusu hili maoni yetu ni kwamba wahusika wanaojihusisha na Ukahaba bila kujali jinsia zao kuwa ni wanawake au wanaume wote ni makahaba tu. Kwa mtazamo huo, watunzi wa riwaya teule wamewatumia wahusika wa kike pekee katika kusawiri suala la Ukahaba katika riwaya zao.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu ulichunguza suala la Ukahaba katika riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini.* Lengo kuu ni kuangalia usawiri wa suala hili katika riwaya na uhalisia wake katika jamii. Kwa hakika kipengele hiki cha kulinganisha suala la Ukahaba katika riwaya na uhalisia wake katika jamii, tafiti zilizotangulia zilikikwepa. Utafiti huu umebainisha kuwa usawiri wa suala la Ukahaba katika riwaya hizi ni tofauti kwa kiasi fulani na uhalisi wake katika jamii.

Kwa mfano, katika riwaya zote mbili, waandishi wanawachora baadhi ya wahusika wakijihulisha na Ukahaba lakini hawaoneshi kwa kina athari zinazowapata wahusika hao wala jamii inasemaje kuhusu Ukahaba huo. Katika *Riwaya ya Vuta N'kuvute*, mwandishi anamuonesha mhusika Yasmin akifanya Ukahaba na Denge hadi anafikia kubeba mimba ya nje ya ndoa lakini mwandishi haoneshi matatizo yaliyompata Yasmin baada ya kubeba mimba hadi kujifungua mtoto huyo.

Vilevile, katika *Riwaya ya Tata za Asumini,* mwandishi anamuonesha mhusika Zaina akijihusisha na Ukahaba kwa kufanya mapenzi na wanaume mbalimbali lakini haoneshi matatizo anayoweza kuyapata mwanamke kahaba kama Zaina. Pia riwaya zote mbili hazioneshi wahusika wanaume kama nao wanaweza ni makahaba zaidi ya wao kuonekana watu wanaokamilisha matamanio ya miili yao. Hali hiyo ni kinyume na uhalisi wake katika jamii kwa sababu jamii inaonesha kuwa suala la Ukahaba halikubaliki hivyo wanawalaani makahaba wa aina zote wawe wanawake au wanaume. Licha ya wanajamii kuwavumilia makahaba, lakini katika hali halisi wanajamii walio wengi wanalaani vitendo hivyo na kuwachukia wahusika hao katika jamii inayohusika.

Kwa sababu hiyo, ni wazi kuwa waandishi wa *Riwaya ya Vuta N'kuvute* na *Tata za Asumini* wamekwepa uhalisia kwa kiasi fulani katika kusawiri suala la Ukahaba katika kazi zao kwa kuwa hazitoi mafunzo ya kutosha kuhusu suala la athari za Ukahaba kwa wahusika na jamii kwa ujumla. Jambo ambalo linaweza kuwafanya baadhi ya wasomaji riwaya, hususani vijana kuona kuwa kufanya Ukahaba ni suala jepesi na linalokubalika katika jamii.

5.4 Mapendekezo

Kwa hakika, hakuna utafiti ambao unaweza kuchukuliwa kuwa umekamisha kila kitu katika eneo ulilolitafiti. Kwa sababu hiyo, ni wazi kwamba utafiti huu haujakamilisha kila kitu katika eneo ulilolichunguza. Hivyo yawezekana kuwa kuna baadhi ya vipengele havijashughulikiwa kwa kina. Kwa hivyo utafiti zaidi unahitajika kuchunguza suala la Ukahaba katika kazi nyingine za fasihi andishi.

Kwa kuwa suala la Ukahaba limeshamiri katika jamii na wala halikubaliki katika jamii hizo kutokana na athari zinazoweza kuwapata wahusika, jamii na taifa kwa ujumla, tunapendekeza uchunguzi zaidi ufanyike katika maeneo au mambo yafuatayo:-

Kwanza, utafiti kama huu unaweza kufanyika kuchunguza usawiri wa Ukahaba katika utanzu mwingine wa fasihi andishi. Kwa mfano, uchunguzi unaweza kufanywa kuchunguza Ukahaba katika tamthiliya za Kiswahili ili kuchunguza uhalisia wa suala hili katika tamthiliya hizo na ukweli wake katika jamii inayohusika.

Pili, tunapendekeza ufanyike utafiti linganishi kuhusu usawiri wa Ukahaba katika kazi za fasihi. Uchunguzi huo ulinganishe usawiri wa suala hili katika utanzu wa

riwaya na tamthiliya ili kubaini kulingana na kutofautiana katika kusawiri suala hili baina ya waandishi wa riwaya na wale wa tamthiliya.

Tatu, utafiti mwingine unaweza kufanywa katika kazi hizi hizi za fasihi andishi lakini mtafiti ateue waandishi kutoka maeneo mbalimbali ya kijiografia. Kwa mfano, mwandishi anaweza kuchagua waandishi wawili wa Kenya na wawili wa Tanzania ili kuzilinganisha kazi zao na kuona waandishi wapi wamelibainisha zaidi suala la Ukahaba katika kazi zao.

Kufanyika kwa tafiti hizo au nyingine kuhusu suala la Ukahaba katika fasihi ya Kiswahili, kutasaidia kuliweka bayana zaidi suala hili katika jamii. Jambo ambalo linaweza kuwasaidia waandishi au watunzi wa kazi za fasihi kulibainisha kwa mapana na marefu suala la Ukahaba katika jamii zao.

MAREJELEO

Bakwasegha, C. (1982), *Profiles of Urban Prostitution: A case study from Uganda.* Kenya Literature Bureau: Nairobi.

Cohen, L. Manion, L. na Morrison, K. (2000), *Research Methods in Education*. New York: Routledge Falmer.

Enon, J. C. (1998), *Education Research, Statistics and Measurements*. Kampala: Makerere University.

Freud, S. (1924), *Introductory Lectures on Psychoanalysis.* Penguin Book.

Gibbe, A. G. (1978). "Dhima ya Mhakiki ", ktk: Mulika.Dar es Salaam: TUKI. Juzuu la 12.

Gibbe, A. G. (1978). "Fasihi na Jamii: Baadhi ya Washairi wa Kiswahili 1960-1977" ktk. Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI. Juzuu la 48/1.

Hegel, G. W. F. (1971), *Introduction to Aesthetics.* Oxford: Clarendon.

Jilala, H. (2016), *Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi.* Dar es Salaam: Daud Publishers Limited.

Kauti, J. M. (2013), "Mabadiliko ya Dhamira Katika Nyimbo za Makuzi ya Mwanamke wa Kiyao". Tasnifu ya M.A. Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (2006), *Utandawazi, Kiswahili na Dhana ya Wakati*. Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI 2005. Dar es Salaam, TUKI.

Kezilahabi, E. (1975). *Shaaban Robert: Mwandishi wa Riwaya*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

King'ei, K & Kisovi, C. N. M. (2005), *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi, Kenya Literature Bureau.

Kishtainy, K. (1982), *The Prostitute in Progressive Literature.* Allinson and Busby Ltd: London.

Kombo, D. K. na Tromp, D. L. A. (2006), *Proposal and Thesis Writting: An Introduction.* Nairobi: Pouliness Publications.

Kothari, C. R (1990) *Research Methodology: Methods and Techniques.*New Age International (P). New Delhi India.

Kothari, C. R (2004) *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Age International (P). New Delhi India.

Libiu, O. S (2012), "Riwaya Mpya ya Kiswahili na Masuluhisho ya Changamoto za Utandawazi". Tasnifu ya M. A Kiswahili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Little, K. (1973), *African Women in Towns.* Cambridge University Press.

Lyatuu, J. (2011), "Usawiri wa Mwanamke Katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Mwandishi wa Kike na wa Kiume Uchunguzi Katika Riwaya Teule". Tasnifu ya M. A. Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mabala, R. S. (1993)."Mchango wa Waandishi wa Riwaya", ktk: Fasihi, Uandishi na Uchapishaji. Dar es Salaam: DUP.

Madumulla, J. S. (1988)."Riwaya ya Kiswahili (Tanzania) katika Miaka ya Themanini", katika: Mulika. Dar es Salaam: TUKI.

Madumulla, J. S. (1987). "Maendeleo ya Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili Tanzania", ktk: Kiswahili. Dar es Salaam:TUKI.

Madumulla, J. S. (1993)."Mwandishi wa Riwaya: Ukweli kuhusu Maisha", katika: Mulika. Dar es Salaam: TUKI.

Masebo, J.A & Nyangwine, N. (2003), *Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili 2.* Dar es Salaam Nyambari Nyangwine Publishers Limited.

Mhilu, G, Nyangwine, N na Kanyuma, Y. (2013). *TAHAKIKI: Vitabu Teule vya Fasihi, Kidato cha 3 na 4.* Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers..

Mlacha, S.A.K. (1993). *Kiswahili Novels and Society.* Dar es Salaam University Press.

Mlacha, S.A.K. (1984). "Riwaya za Visiwani (1970-1980) na Ujenzi wa Jamii Mpya", katika *Mulika*. Dar es Salaam: TUKI.

Mlacha, S.A.K. (1985). "Wahusika katika Riwaya za Kiswahili Tanzania (1970-1982)", ktk: Mulika. Dar es Salaam: TUKI. Juzuu la 17.

Mligo, E. S. (2012), *Jifunze Utafiti. Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering EGYS.

Mohamed, S. A (1990). *Tata za Asumini.* Longhorn Publishers , Nairobi.

Muga, E. (1980), *Studies in Prostitution: East, West and South Africa, Zaire and Naveda*. Kenya Literature Bureau: Nairobi.

Mulokozi, M. M. (1996), *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Mutembei, A. K. (2000), "Fasihi ya Kitaifa na Fasihi ya Kiswahili ni Dhana Ileile?" Katika Mulika. Dar es Salaam: TUKI

Nguma, N. (2001). Taswira ya Mwanamke Jinsi Ilivyochorwa Katika Riwaya ya Kezilahabi. (Tasnifu ya uzamili, haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Njogu, K na Chimerah R. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Omar, S. (2009), "Tanzania Hip Hop Poetry as Popular Literature". (Tasnifu ya uzamili, haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ntarangwi, M. (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College

Padgett, D. (2002). *Qualitative Methods in Social Work Research: Challenges and Rewards*. London: Sage Publications Inc.

Senkoro, F. E. M. K. (1982), *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre

Senkoro, F.E.M.K. (1982). "Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili", katika: *Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaam Press and Publicity Centre.

Shafi, S. A. (1999). *Vuta N'kuvute.* Dar es Salaam. Oxford University Press.

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press

Wafula, R. M na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* JKF, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi, Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2010), *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers

Wellek, R. (1961). *"The Concept of Realism in Literary Scholarship".* Neophilologus: Penguin.

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

KITIVO CHA FANI NA SAYANSI ZA JAMII

IDARA YA ISIMU NA TAALIMU ZA KIFASIHI

I. MASWALI YA MWONGOZO KWA WAHOJIWA WATU WAZIMA

1. Je katika eneo hili kuna wanajamii wanaojishughulisha na Ukahaba?
2. Unadhani kwa nini watu hao wanajiingiza katika vitendo vya Ukahaba?
3. Athari gani anazozipata mtu anayejiingiza katika vitendo cha Ukahaba?
4. Jamii inapata athari gani watu wake wanapojiingiza katika vitendo vya Ukahaba?
5. Jamii ina mtazamo gani juu ya watu wake kujiingiza katika Ukahaba?
6. Nini kifanyike kuzuia Ukahaba katika jamii?

Ahsante kwa msaada wako

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

KITIVO CHA FANI NA SAYANSI ZA JAMII

IDARA YA ISIMU NA TAALIMU ZA KIFASIHI

II. HOJAJI YA VIJANA

MAELEZO:

- ✓ *Yote utakayoyaeleza humu yatakuwa siri baina ya wewe na mimi.*
- ✓ *Tafadhali majibu yako yawe ya kweli ili kupata tathmini za uhakika.*
- ✓ *Weka alama ☑ panapohusika.*

1 Je, kuna mtu au watu wanaojishughulisha na Ukahaba katika mtaa unaoishi?

Ndio ☐ Hapana ☐

2 Unadhani kwa nini anafanya au wanafanya Ukahaba? Toa sababu tatu (3).

.....

.....

.....

3 Je, kuna athari au matatizo yoyote anayopata mtu anayejishughulisha na Ukahaba?

Ndio ☐ Hapana ☐

4 Taja matatizo matatu anayoweza kuyapata mtu anayejiingiza katika Ukahaba.

.....

.....

.....

5 Je, unamchukuliaje mtu huyo? (Anafanya kosa au ni hali ya kawaida).

.....

.....

.....

6 Je, kuna athari au matatizo yoyote yanayoweza kumpata mwanamke anayejishughulisha na Ukahaba?

Ndio ☐ Hapana ☐

7 Taja japo matatizo matatu ikiwa yapo.

.....

.....

.....

8 Taja athari mbili (2) ikiwa zipo zilizompata mwanaume anayejishughulisha na Ukahaba?

.....

.....

9 Unaonaje mtu anayejishughulisha na Ukahaba wa kawaida au ni mzigo kwa jamii?

.....

.....

.....

10 Toa mapendekezo yako. Nini kifanyike kuzuia tatizo la Ukahaba katika jamii?

.....

.....

.....

.....

Ahsante kwa Msaada wako